# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# TUME YA MIPANGO ZANZIBAR

# MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023
# NA MPANGO WA MAENDELEO 2023/2024

## KITABU CHA PILI

**JUNI, 2023**

# YALIYOMO

**Mada** **Ukurasa**


**YALIYOMO:.........................................................................................i**

**1.0 UTANGULIZI .......................................................................................1**

**2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023..........2**
2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia .......................................................2
2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika.......................................................2
2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa
2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki..................................3
2.5 Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei wa Dunia........................................3

**3.0 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2023 ..........................4**
3.1 Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar ...........................................5

**4.0 MALENGO NA SHABAHA YA UCHUMI JUMUISHI KWA MWAKA 2023/2024 ......................................................................................6**
**5.0 MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024 ........................................................................................6**
**6.0 MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2023/2024 ......................7**
**7.0 RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024................8**
**8.0 MWELEKEO WA PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2023/2024 .......................................................................................9**
8.1 Ofisi ya Rais Ikulu ..........................................................................9
8.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji .......................................10
8.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango ...................................................11
8.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar .......................................................14
8.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ........................................16
8.4 Ofisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora .................18
8.4.1 Mahakama Kuu .........................................................................19
8.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ .........................................................................................21
8.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ...................22
8.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ..........................23
8.5.3 Kikosi cha Valantia.....................................................................23

8.5.4 Chuo cha Mafunzo ..........................................................................24
8.5.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi .................................................25
8.6 Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais...............................................26
8.6.1 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya..29
8.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ...............................................................................................30
8.8 Wizara ya Afya ....................................................................................31
8.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi........................................36
8.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda................................37
8.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.............................................38
8.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ...........................41
8.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.......................41
8.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ................46
8.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini...................................................47
8.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ............................................52
8.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ..................................60
8.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale .................................................65

**9. MIRADI YA MAENDELEO INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KUPITIA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA........................................................................................65**
**10.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI......................................................66**
**11.0 WASHIRIKA WA MAENDELEO.....................................................66**
**12.0 HITIMISHO......................................................................................67**

## 1.0 UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024 ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 pamoja na Sera na Mipango ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda, na Kimataifa. Maendeleo Endelevu yanategemea ushirikiano wa wadau wote ikiwemo Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Wananchi kwa pamoja wana wajibu wa kujenga uchumi na kulinda rasilimali zilizopo.

Juhudi za kukuza uchumi jumuishi zitaendelezwa kwa mujibu wa takwimu za awali matarajio ya ukuaji wa uchumi utakuwa ni wastani wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2023. Maeneo yanayotarajiwa kukuza uchumi ni pamoja na kuanza utekelezaji na usimamizi wa Miradi mikubwa ya Kimkakati itakayotoa matokeo chanya kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na Ujenzi wa miundombinu ya usafiri; Uimarishaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu; Ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama pamoja na Ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya. Makadirio yanaonesha kuwa kasi ya mfumuko wa bei itabakia katika tarakimu moja. Kutakuwa na ongezeko la miradi ya uwekezaji kutokana na hatua za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi binafsi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje. Aidha, uimarishaji wa Utawala Bora, Mshikamano na Umoja wa Kitaifa utaimarishwa kwa kuweka msisitizo wa kuimarisha demokrasia, kutii sheria na uwajibikaji ili amani na utulivu kuendelea kuwepo Zanzibar na hatimae kuwa na uchumi endelevu.

Udhibiti wa matumizi ya rasilimali fedha kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 utakuwa wa karibu sana kutokana na changamoto za upatikanaji wake hasa kwa upande wa fedha za Washirika wa Maendeleo. Fedha za programu na miradi ya maendeleo zitatumika kwa miradi yenye kuleta tija, kukamilisha miradi inayoendelea na uanzishwaji wa miradi mengine ya maendeleo. Serikali itaweka mikakati maalum ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024 na itaendelea kufanya juhudi ya kutoa taarifa kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo.

Kitabu hiki kinaelezea Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 kwa kutekeleza malengo

yaliyoainishwa katika Mikakati ya Maendeleo ya Kitaifa, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs) 2030, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa mwezi wa Novemba 2020 wakati akizundua Baraza la kumi la Wawakilishi.

## 2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023

### 2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia.

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi wa Aprili 2023 kasi ya ukuaji wa uchumi wa Duniani ni ukuaji wa kasi ndogo kufikia wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2022. Matarajio ya kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa Dunia itatokana na athari za vita vinavyoendelea baina ya nchi ya Urusi na nchi ya Ukraine ambavyo vimeathiri sekta za uzalishaji zikiwemo mafuta na gesi na kusababisha kuongezeka gharama za usafirishaji wa bidhaa duniani.

Kwa Nchi Zilizoendelea, kasi ya ukuaji inatarajiwa kukua kwa kasi ndogo kufikia wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2023, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.7 mwaka 2022. Uchumi wa Umoja wa Ulaya unatarajiwa kuwa na ukuaji hasi wa wastani wa asilimia 0.3 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 4.0 mwaka 2022.

Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi (Emerging Market and Developing Economies), kasi ya ukuaji inatarajiwa kufikia asilimia 3.9 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 4.0 mwaka 2022. Hata hivyo ukuaji wa uchumi wa Nchi za Afrika Mashariki uchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2022.

### 2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika

Kwa mwaka 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi Barani Afrika inatarajiwa kupanda na kufikia wastani wa asilimia 4.0 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022. Ukuaji huu utatokana na kuongezeka kwa uuzaji wa malighafi zinazozalishwa Afrika katika soko la nje kama vile nchi ya Nigeria na Libya wanatarajia kuongeza uuzaji wa mafuta katika soko hilo. Hivyo, hali hii itasaidia ukuaji wa uchumi wa nchi za Bara la Afrika kwa ujumla. Aidha, mabadiliko hayo yatapelekea muelekeo mpya wa masoko mbadala ya chakula, nishati na rasilimali za madini kuelekea mabadiliko ya uchumi wa kijani.

## 2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Hali ya uchumi wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika Ukanda huu kunatokana na kupungua kwa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambao utapelekea kupungua kwa upatikanaji wa fedha na kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi.

## 2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki mwaka 2023 inatarajiwa kuimarika na kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 5.4 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2022.

Kwa mwaka 2023, Uchumi wa Jamhuri ya Muungano wa **Tanzania**, unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.7 ya mwaka 2022. **Uganda** unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.7 kwa mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2022, nchi ya **Burundi** uchumi unatarajiwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 3.3 kwa mwaka 2023 kutoka asilimia 1.8 mwaka 2022.

Hata hivyo, uchumi wa nchi ya **Kenya na Rwanda** unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo mwaka 2023. Uchumi wa Kenya unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo kufikia wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2023 kutoka asilimia 5.4 mwaka 2022. Ukuaji huo mdogo wa uchumi wa Kenya utatokana na kupungua kwa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inaathiri uwezo wa nchi kuwekeza katika afya, elimu na miundombinu na kupelekea ukuaji mdogo wa uchumi. Kwa upande wa nchi ya Rwanda, Ukuaji wa uchumi wa Rwanda unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 6.2 mwaka 2023 kutoka asilimia 6.8 mwaka 2022.-

## 2.5 Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kasi ya mfumuko wa bei Duniani inatarajiwa kupungua hadi kufikia wastani wa asilimia 7.0 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022. Makadirio ya kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei Duniani kutatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za nishati ya mafuta na bidhaa za chakula na kuimarika kwa Sera za Kifedha Duniani.

Kwa Nchi Zilizoendelea kasi ya mfumuko wa bei inatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 4.7 kwa mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022 na Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 8.6 kwa mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2022.

## 3.0 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2023

Mwelekeo wa hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2023 unatarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano 2021-2026 (ZADEP); Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025 na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati akilihutubia rasmi Baraza hili la kumi mwezi wa Novemba 2020. Mpango huu umezingatia pia Sera na Mikakati ya Kisekta; Kikanda na Kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030.

Vile vile, Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia misingi ya mipango ya awali iliyolenga kuimarisha na kukuza uchumi jumuishi wenye kuhimili ushindani.

Kwa mwaka 2023, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.1 kutoka ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2022 matarajio ya ukuaji huo utatokana na sababu zifuatazo:-

i Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 30 wanaotarajiwa kufikia watalii 713,053 mwaka 2023 kutoka watalii 548,503 kwa mwaka 2022;

ii Kuendelea kutekelezwa kwa Miradi mikubwa na ya Kimkakati ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani na ukarabati wa Bandari ya Malindi. Miradi mengine itakayochangia ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ubaki katika tarakimu moja;

iv Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali;
v Kuongezeka kwa hatua za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi binafsi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje; na
vi Kufanya mageuzi ya Sekta ya Kilimo ili kuongeza uzalishaji, uongezaji thamani na masoko pamoja na kufanya mageuzi kwa kuimarisha mazao viungo ikiwemo karafuu, mwani na nazi.

Matarajio ya Ukuaji wa Uchumi Unatengemea na Misingi ifuatayo:

i Kuendelea kuimarisha mifumo ya kifedha na kuongeza makusanyo ya ndani;
ii Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;
iii Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama nchini na kwa nchi jirani; na
iv Kuendelea kuimarika miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu.

### 3.1 Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar

Kwa mwaka 2023 makadirio ya hali ya mfumuko wa bei wa Zanzibar yanaonesha kuwa kasi ya mfumuko wa bei wa Zanzibar itapungua na itaendelea kubakia katika tarakimu moja na inakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 4.5 kutoka 5.1 kwa mwaka 2022 Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa kuweka utulivu wa bei ikiwa ni pamoja na:

i. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;
ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei;
iii. Kuimarisha programu za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa ndani wa chakula;
iv. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine;
v. Kuendelea kushajiisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani;
vi. Kuimarika kwa huduma za Bandari ya Malindi baada ya kuingia ubia wa bandari wa uendeshaji na sekta binafsi;

vii. Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini; na
viii. Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku.

## 4.0 MALENGO NA SHABAHA YA UCHUMI JUMUISHI KWA MWAKA 2023/2024

Shabaha za Uchumi Jumuishi zilizozingatiwa katika Mpango wa mwaka 2023/2024, ni kama ifuatavyo:-

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2023;
ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kubakia katika tarakimu moja;
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 26.0 ya Pato la Taifa mwaka 2023/2024 kutoka wastani wa asilimia 24.7 ya mwaka 2022/23;
iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 22.0 ya Pato la Taifa mwaka 2023/2024 kutoka asilimia 18.1 mwaka 2022/23; na
v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## 5.0 MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024

Kwa kipindi cha mwaka 2023/2024, Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo utaendelea kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 kupitia programu na miradi ya kimkakati, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la kumi (10) la Wawakilishi. Maelekezo ya Serikali kiujumla pamoja na ahadi zilizotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na ziara za makundi mbali mbali pamoja na miongozo iliyotolewa kwa viongozi wakuu kupitia sekta tofauti nayo imezingatiwa. Lengo ni kuiwezesha Serikali kufikia azma ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs) 2030 ili kuweza Kukuza Uchumi wa Zanzibar.

Mpango huu wa mwaka 2023/2024, utaendelea kuimarisha maeneo ya kukuza uchumi na ustawi wa kijamii kwa ujenzi wa miundimbinu ya usafiri (ikiwemo bandari, barabara na viwanja vya ndege), kuimarisha uchumi wa buluu, ubora wa elimu, huduma za afya na upatikanaji wa maji safi na salama, mazingira bila ya kusahau huduma nyengine stahiki za kijamii na masuala ya utawala bora nchini. Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kwa mwaka 2023/2024, utasaidia katika kuimarisha hali za wananchi, kuongeza uwekezaji, kuongeza uwezo wa rasilimali watu, kukuza ajira na hatimae kuongeza mapato ya Serikali ili kuwezesha kuleta matokeo chanya na ya haraka katika kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana kwa viwango stahiki pamoja na kukuza shughuli za kiuchumi.

## 6.0 MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2023/2024

Katika Mpango wa Maendeleo wa 2023/2024 Serikali imedhamiria kutekeleza miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi yenye lengo la kuimarisha Ukuzaji wa Uchumi, miundombinu, huduma za jamii na utawala bora. Kwa kuzingatia maeneo hayo, programu na miradi ya kimkakati inayotarajiwa kutekelezwa ni ifuatayo:-

i. **Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu**
   - a) Ujenzi wa Bandari za Uvuvi katika eneo la Mangapwani;
   - b) Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki katika eneo la Kama.

ii. **Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu**
   - a) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Karume - Pemba;
   - b) Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani;
   - c) Kuimarisha bandari za Malindi, Wete na Mkoani;
   - d) Ujenzi wa Barabara Kuu (km 407.6) na Barabara za Ndani (km 275.9);
   - e) Matengenezo ya Barabara za Mjini (km 100.9); na
   - f) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati.

iii. **Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii**
   - a) Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo;
   - b) Ujenzi na Uimarishaji wa Nyumba za Madaktari;
   - c) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Binguni;

d) Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu;

e) Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji wa Maji Safi na Salama; na

f) Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar (Boost Inclusive Growth in Zanzibar - BIG-Z).

iv. **Utawala Bora na Uhimilivu**

a) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama; na

c) Ujenzi wa Mji wa Serikali.

## 7.0 RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024

Serikali kwa mwaka 2023/2024 imepanga kutumika TZS 1,521.99 bilioni kwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo ambapo TZS 1,514.79 bilioni zitatumika kwa miradi ya maendeleo katika Serikali Kuu na TZS 7.2 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Fedha hizo (TZS 1,514.79 bilioni) za Serikali Kuu zinajumuisha TZS 886.0 bilioni sawa na asilimia 58.2 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka Serikalini na TZS 628.79 bilioni (TZS 101.24 bilioni Ruzuku na TZS 527.55 ni Mkopo) sawa na asilimia 41.3 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Serikali (TZS 886.0 bilioni), TZS 144.0 bilioni ni kwa ajili ya Mfuko wa Huduma ya Mikopo kwa Miradi ya Maendeleo – "Debt Service Fund".

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 unalenga kutekeleza jumla ya programu 31(Programu 3 mpya) na miradi ya maendeleo 58 (19 ni miradi mipya) itakayogharimu TZS 1,514.79 bilioni ikiwa ni ongezeko la TZS 162.60 bilioni sawa na asilimia 12.0 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2022/23 ya TZS 1,352.19 bilioni. Kati ya fedha hizo za maendeleo, TZS 915.87 bilioni sawa na asilimia 60.46 zimepangwa kutumika kwa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Kimkakati na TZS 454.92 bilioni sawa na asilimia 30.03 ni kwa Miradi Mengineyo inayojumuisha miradi inayoendelea na ile ambayo Serikali ina dhima kwa Washirika wa Maendeleo.

Mgawanyo wa makisio ya fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo Kiwizara kwa programu na miradi ya maendeleo unaonekana kwenye **Kiambatisho nambari 1.**

## 8.0 MWELEKEO WA PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2023/2024

### 8.1 Ofisi ya Rais Ikulu

Ofisi ya Rais Ikulu ina jukumu la kusimamia majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi ili kuhakikisha jamii inapata uelewa juu ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo na sera zinazotekelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia, Ofisi ina wajibu wa kuratibu shughuli za Wazanzibar wanaoishi Nje ya nchi (Diaspora). Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi imepanga kutekeleza miradi mitatu ya Maendeleo kwa gharama ya TZS 7.9 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha makaazi ya viongozi wa nchi na kuyaweka makaazi hayo katika mandhari na mazingira mazuri ili kuzipa hadhi na kuimarisha usalama wa nyumba hizo. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.4 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujenga uzio katika Ikulu ndogo ya Dodoma;
ii. Kufanya matengenezo ya Ikulu ndogo ya Mkoani – Pemba;
iii. Kukamilisha ujenzi wa Ikulu ndogo ya Dar es salaam; na
iv. Kufanya matengenezo ya Ikulu ya Mnazi Mmoja.

***Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais***

Mradi huu una lengo la kuimarisha ulinzi na usalama katika majengo ya Ikulu na makaazi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuhakikisha kunapatikana miundombinu iliyo imara ya mifumo ya ulinzi na usalama katika majengo hayo. Mradi umeanza mwaka 2022/2023 na unatarajiwa kukamilika 2024/2025 ambapo kwa mwaka 2023/2024, umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Utafutaji na ufungaji wa mfumo wa mtandao katika maeneo ya Ikulu;
ii. Utafutaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA (ICT);

iii. Kufunga CCTV Camera katika Ikulu ndogo ya Dar es Salaam, Pemba na Dodoma; na
iv. Kutoa mafunzo yanayohusiana na TEHAMA (ICT) kwa watumishi wa Ofisi.

***Mradi wa Uimarishaji wa Shughuli za Taasisi za Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar.***

Mradi huu una lengo la kuhakikisha upatikanaji wa jengo la kisasa kwa Taasisi za kuhifadhia nyaraka za Serikali ili kuimarisha mfumo wa uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu. Mradi unatarajiwa kuanza mwaka 2023/2024, ambapo umepangiwa kiasi cha TZS 4.5 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli iliyopangwa kutekelezwa mwaka 2023/2024***

- Kuanza na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Nyaraka katika eneo la Kilimani.

**8.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji**

Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji inasimamia Idara na Taasisi ambazo zina jukumu la kutekeleza malengo ya Wizara ambayo ni pamoja na kusimamia upatikanaji wa kazi za staha na kuzingatia sheria na viwango vya kazi, kuimariasha hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar pamoja na kuimarisha na kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi. Aidha, Sekta hii inatekeleza shughuli zake kupitia mipango na mikakati ya kimaendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 10.5 bilioni.

***Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo, Wakati na Wakubwa***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kupunguza umasikini kwa kuwawezesha wajasiriamali wadogo, wakati na wakubwa kuongeza ajira, kukuza kipato na kusaidia kujitegemea kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Abudhabi kupitia Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund) na unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2022 - 2027). Kwa mwaka 2023/2024, mradi umetengewa jumla ya TZS 7.0 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 4.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 2.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali*

i. Kuwajengea uwezo Wajasiriamali na watendaji wa Taasisi;
ii. Ujenzi wa mindombinu ya Wajasiriamali; na
iii. Usimamizi na uratibu wa mradi.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Washirika wa Maendele*

i. Kutoa mikopo kwa Wajasiriamali; na
ii. Kuwajengea uwezo Wajasiriamali wadogo, wakati na wakubwa.

*Mradi wa Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji*

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2021/22 kwa lengo la kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika maeneo yote yalioainishwa kwa uwekezaji ambapo miundombinu muhimu ikiwemo barabara, maji na umeme itawekwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Mradi huu unatekelezwa na Serikali na unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22 – 2025/26). Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.5 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ujenzi wa ukuta na nyumba ya walinzi katika maeneo huru ya uwekezaji Micheweni; na
ii. Upelekaji wa miundombinu katika maeneo ya uwekezaji Micheweni.

**8.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango**

Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ina majukumu ya kusimamia shughuli zote zinazohusiana na mapato na matumizi ya fedha za Serikali, shughuli za kiuchumi na mipango ya kimaendeleo, kusimamia maendeleo ya Taasisi za kifedha zikiwemo Benki, Bima na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Aidha, Ofisi hii ina wajibu wa kuishauri Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu mapato ya nchi ikiwemo ukusanyaji wa kodi, tozo na mapato yatokanayo na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi hii imepangiwa jumla ya TZS 102.90 bilioni (TZS 74.2 bilioni kutoka Serikalini na TZS 28.6 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kuteleza programu tatu na miradi miwili ya maendeleo.

***Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar***

Programu hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Programu imepanga kujenga Ofisi mpya katika maeneo ambayo yamependekezwa na Serikali na kukarabati majengo ambayo yameonekana kuchakaa au kupungua nafasi katika Ofisi hizo. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 74.12 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ukamilishaji wa kazi ya utanuzi na ujenzi wa Ofisi za Serikali ikiwemo: Skuli ya Sheria, Ofisi ya Mufti, Nyumba ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais, Ofisi ya Shirika la Magazeti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA), Tume ya Utangazaji na Tume ya Uchaguzi; na
ii. Kuanza ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka - Unguja.

***Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)***

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar inalenga kuimarisha miundombinu na huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Programu hii inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021-2026) kwa gharama za jumla ya TZS 346.5 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 22.810 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa vifaa vya usafi (magari ya taka, makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara) kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa za Unguja na Pemba;
ii. Kufanya mapitio ya usarifu wa michoro na kuanza matayarisho ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa kuendeleza eneo la Michenzani na mradi salama wa watembea kwa miguu Mji Mkongwe;
iii. Ununuzi wa vifaa vya uchunguzi vya maabara ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS);
iv. Kuzijengea uwezo Taasisi za Serikali zinazosimamia maendeleo ya Miji pamoja na ununuzi wa vitendea kazi;

v. Kutayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi Pemba (Pemba Master Plan); na
vi. Kuanza kazi za ujenzi wa mitaro na barabara za ndani kwa Unguja na kukamilisha usarifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua na barabara za ndani kwa Pemba.

***Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP – V)***

Programu hii ina lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Programu imeanzishwa mwaka 2017/2018 na imekadiriwa kutumia jumla ya TZS 8.80 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, Programu imepangiwa jumla ya TZS 3.89 bilioni ambapo TZS 128.40 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.76 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji wa programu; na
ii. Kutoa huduma za uratibu wa Mradi.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kutoa mafunzo ya uchunguzi wa kodi, vihatarishi na uchambuzi wa sera za kodi na mapato kwa watumishi wa Taasisi zinazohusiana na kodi;
ii. Kuimarisha na kuanzisha mifumo inayohusiana na usimamizi wa kodi, ukaguzi pamoja na usimamizi wa mipango na bajeti;
iii. Kufanya mapitio na kutoa miongozo inayohusiana na sheria mbali mbali za mapato, matumizi, udhibiti na ukaguzi;
iv. Kuwajengea uwezo watumishi mbali mbali kuhusiana na mipango, udhibiti, ukaguzi na usimamizi wa fedha za umma; na
v. Kufanya ziara za kujifunza ili kuongeza uwelewa juu ya usimamizi wa fedha za umma na udhibiti.

***Mradi wa Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili***

Lengo la mradi huu ni kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili. Mradi umeanza mwaka 2016/2017 na umekadiriwa kutumia jumla ya TZS 6.20 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, Mradi huu umepangiwa kutumia TZS 1.72 bilioni (TZS 34.70 milioni kutoka Serikalini na TZS 1.69 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Kutoa huduma za uratibu na usimamizi wa mradi.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Huduma za ushauri kwa kuandaa Mkakati, Sera, Sheria ya Madini Zanzibar na Kanuni zake;
ii. Kujenga uwezo juu ya Mkakati, Sera, Sheria na Kanuni za Madini Zanzibar;
iii. Huduma za ushauri kwa ajili ya mapitio ya rasimu ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta (PRMA) ikiwa ni pamoja na Kanuni za Governemnt Financial Statistics (GFS) za Mafuta na Gesi;
iv. Huduma za ushauri kwa maendeleo na Rasimu ya Sheria ya Ushuru wa Mafuta, ikiwa ni pamoja na Ushuru wa Faida ya Ziada;
v. Kujenga uwezo kuhusu uanzishwaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Petroli; na
vi. Kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya uanzishwaji wa Sheria ya Kodi ya Mafuta (Petroli).

**8.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar**

Tume ya Mipango ni chombo cha juu chenye mamlaka ya kuratibu, uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, ikiwemo mipango ya maendeleo ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi; kuratibu masuala ya kiuchumi kitaifa, kikanda na kimataifa, uandaaji wa tafiti mbali mbali pamoja na kushughulikia masuala ya idadi ya watu na mipango ya watenda kazi. Aidha, Tume hushughulikia uratibu na upangaji wa vipaumbele vya nchi na kutoa miongozo mbali mbali ya kimaendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, Tume ya Mipango ya Zanzibar imepangiwa jumla ya TZS 6.0 bilioni (TZS 5.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 500 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza Programu moja na miradi miwili ya maendeleo.

***Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar***

Programu hii imelenga kukamilisha shughuli za urasimishaji wa ardhi na biashara Zanzibar ili ziweze kutumika katika juhudi za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa Programu hii utawawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na kuendesha biashara nje ya mfumo usio rasmi waweze

kuzirasimisha, kuzitumia na kupata mitaji kwa ajili ya kushiriki katika uchumi wa kisasa ulio rasmi. Kwa mwaka 2022/2023, Programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 2.5 bilioni (TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini na 500 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya utambuzi wa ardhi katika maeneo ya Mombasa kwa Mchina, Kidoti, Mahonda, Fuoni na Amani kwa upande wa Unguja, Utaani na Micheweni kwa upande wa Pemba;
ii. Kutayarisha na kuchapisha hati za usajili kwa maeneo yaliyotambuliwa;
iii. Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Hati za Matumizi ya Ardhi;
iv. Kutoa mafunzo na kuwahakiki wafanyabiashara wadogo 150 kwa kila Wilaya Unguja na Pemba;
v. Kuanzisha vituo jumuishi viwili vya urasimishaji biashara (Wilaya ya Kati na Wilaya ya Wete);
vi. Kutoa elimu ya uhamasishaji na kushiriki maonyesho mbali mbali ya kibiashara; na
vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za mradi.

***Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi***

Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi una lengo la kuimarisha uandaaji na utayarishaji wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa programu na miradi ya maendeleo. Mradi huu kwa awamu ya kwanza utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2022/23-2024/25) na umepangiwa kutumia jumla ya TZS 23.4 bilioni. Ukamilishaji wa mradi huu utarahisisha utekelezaji wa miradi ya Serikali na utafutaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 1.5 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya upembuzi yakinifu kwa programu/miradi ya maendeleo;
ii. Kuandaa mfumo wa ukusanyaji taarifa na ripoti za upembuzi yakinifu kwa programu/miradi ya maendeleo; na
iii. Kujenga uwezo wa Taasisi na watendaji juu ya utayarishaji na uchambuzi wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa programu na miradi ya maendeleo.

***Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa***

Mradi una lengo la kuimarisha Uratibu, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Mradi umepangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2023/2024 hadi 2025/2026 na kwa mwaka 2023/2024, umepangiwa TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kulinganisha viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, Ajenda ya Afrika 2063 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026;
ii. Kujenga uwezo juu ya masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Wizara, Idara, Taasisi na Serikali za Mitaa;
iii. Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (ZDV) 2050;
iv. Kutayarisha na kuchapisha Ufupisho wa Sera (Policy Brief) ya ripoti ya Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka na miezi sita;
v. Kufanya mapitio ya Muda wa Kati ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026;
vi. Kufanya tathmini ya muda wa kati na muda wa mrefu wa programu na miradi ya maendeleo;
vii. Kuandaa Mkakati wa Mawasiliano ya Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026;
viii. Kufanya mapitio ya Mfumo wa Kieletroniki wa Mipango ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Programu na Miradi ya Maendeleo; na
ix. Kuandaa ripoti ya Hiari (VNR) 2023 ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030.

### 8.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Ofisi hii ina jukumu la kuratibu uzalishaji, ukusanyaji, uchambuzi, uchapishaji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa na takwimu zilizo rasmi, kutoa takwimu na taarifa zenye ubora na kuhamasisha matumizi ya takwimu katika mipango ya

maendeleo, kufanya maamuzi katika masuala ya utawala na uendeshaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi imepangiwa jumla ya TZS 4.43 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza Programu moja kuu.

***Mradi wa Uendelezaji Takwimu Zanzibar (ZSDP)***

Mpango wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) ni programu ya Uendelezaji Takwimu kwa matokeo unaolenga kuimarisha takwimu za kawaida (Routine data) sambamba na uimarishaji wa mfumo wa Taifa wa Takwimu. Mpango huu umejikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni; kuhakikisha ubora na uwasilishaji wa taarifa; utoaji wa Takwimu, Uimarishaji na Uendelezaji wa Taasisi; na kuimarisha mifumo ya taarifa za Kiutawala ili iweze kutoa Takwimu kwa lengo la kupunguza gharama za tafiti kubwa.

Utekelezaji wa Mpango huu ni muda wa miaka mitano (2022/23 hadi 2026/27) kwa madhumuni ya kuongeza wigo na mbinu za uwasilishaji wa Takwimu pamoja na kuhamasisha matumizi yake katika nyanja na ngazi zote; teknolojia katika kukusanya na kuchambua taarifa zinazopatikana kutoka katika mifumo mbali mbali; uimarishaji miundombinu ya kitakwimu pamoja na kuwapatia mafunzo watendaji wanaofanya kazi za kitakwimu ndani ya Taasisi za Serikali na kutoka Sekta binafsi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imekadiriwa kutumia jumla TZS 4.43 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya mapitio na kuimarisha Takwimu za Pato la Taifa;
ii. Kufanya Sensa ya Viwanda ya Robo Mwaka na Mwaka 2022 wa Uzalishaji Mali Viwandani;
iii. Kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii ikiwemo Utafiti wa Mwaka wa Kilimo; Utafiti wa Uajiri na Mapato wa Mwaka 2022; Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2023/2024; Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya na Utafiti wa kufuatilia Kaya;
iv. Kukusanya takwimu za mfumuko wa bei katika maeneo mengine ya Mjini na Vijijini;
v. Uratibu wa shughuli za Kitakwimu katika Mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar;
vi. Kuandaa Mkakati wa Uhamasishaji na Mawasiliano;
vii. Kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Usambazaji Takwimu;

viii. Kufanya mapitio ya sheria na kanuni za Takwimu; na
ix. Matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mtakwimu Pemba.

### 8.4 Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Ofisi inasimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za sekta ya Sheria, utumishi na utawala bora Zanzibar. Aidha, Ofisi ina lengo la kuwa na utumishi wa umma ulio imara kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa jamii kwa kuzingatia misingi ya haki, Sheria, demokrasia na utawala bora ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma nzuri na bora kwa wananchi wote. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi imepanga kutekeleza programu mbili na miradi mitatu ya maendeleo kwa gharama ya TZS 29.34 bilioni kati ya fedha hizo TZS 28.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.34 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa Awamu ya II (ZPSRP II)***

Programu hii ina lengo la kukuza uwajibikaji na utendaji kwa watumishi wa umma Zanzibar, kwa kuzingatia taratibu zote za mifumo iliyobora katika utoaji wa huduma kwa ufanisi. Programu imeanza mwaka 2018/2019 na imekadiriwa kutumia jumla ya TZS 12.1 bilioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 750 milioni kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya mapitio ya Mpango wa Mageuzi katika Utumishi wa Umma;
ii. Kuimarisha Mfumo wa Kieletroniki wa usajili wa taarifa za mali na madeni ya Viongozi wa Umma;
iii. Kutayarisha Awamu ya Pili ya Mfumo wa Taarifa za Watumishi wa Umma na Malipo; na
iv. Kutayarisha Mfumo wa Upimaji Utendaji Kazi kwa Wizara za SMZ pamoja na ununuzi wa vifaa.

***Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria***

Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria imeanzishwa mwaka 2022/23 kwa lengo la kuwezesha wananchi kisheria na kuhakikisha upatikanaji wa haki. Programu hii imepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano 2022/23 hadi 2026/27 na itagharimu jumla ya TZS 5.0 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa kiasi cha TZS 1.2 bilioni (TZS 250 milioni kutoka Serikalini na TZS 969 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kufanya mapitio ya sheria zinazosimamiwa na Wizara;
ii. Kutayarisha Mfumo wa Usajili wa Utoaji wa Msaada wa Kisheria pamoja na mafunzo kwa watoa huduma za Msaada wa Kisheria; na
iii. Kutayarisha Jukwaa la Taarifa za Maadili na Uchambuzi.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo.***

i. Kuimarisha mifumo na uwezo wa Taasisi za sheria na rasilimali watu;
ii. Kuziwezesha Asasi za Kiraia kutoa msaada wa kisheria na kuhamasisha jamii juu ya haki za kisheria na za kibinadamu kwa makundi hatarishi; na
iii. Kuanzisha mfumo wa upatikanaji wa haki kwa kesi za unyanyasaji wa kijinsia.

***Mradi wa Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake Katika Kesi za Udhalilishaji (UN-WOMEN)***

Mradi huu una lengo la kupunguza vitendo vya udhalilishaii kwa vijana, wanawake na watoto. Mradi umeanza mwaka 2023/2024 na unatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 373 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikalini.***

i. Kuimarisha uratibu na taratibu za usimamizi wa kesi katika ngazi ya kitaifa kupitia mikutano kati ya polisi, mahakama na DPP;
i. Kuimarisha programu za utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wanawake na watoto;
ii. Kuandaa Miongozo ya Hukumu ya Kimahakama;
iii. Kujenga uwezo wa Kitengo cha Ulinzi cha kesi za jinai cha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (Protection Unit); na
iv. Kufanya Mapitio ya mfumo wa kisheria wa uwezeshaji na ulinzi wa wanawake.

### 8.4.1 Mahakama Kuu

Mahakama kuu ndio chombo cha juu katika kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya jinai na madai ya wananchi yanayowasilishwa mahakamani ili kufanikisha upatikanaji wa haki nchini. Kwa mwaka 2023/2024, Mahakama imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo yenye jumla ya TZS 27.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Mikoa***

Mradi huu una lengo la kujenga majengo ya mahakama za Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya kazi na kuwa na Ofisi za kisasa zitakozoengeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji wa haki. Mradi huu umeanza 2022/2023 na umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano (2022-2027) na utagharimu jumla ya TZS 48.6 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 25 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Mazizini-Unguja;
ii. Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini katika eneo la Pale;
iii. Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja katika eneo la Tunguu/ Binguni;
iv. Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba katika eneo la Kinyasini; na
v. Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kusini Pemba katika eneo la Mfikiwa-Chake Chake.

***Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi***

Mradi umeanzishwa mwaka 2022/23 kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa kesi kwa njia ya kielektroniki ambao utaimarisha utendaji wa kazi za Mahakama katika kutoa huduma na haki kwa wananchi kwa wakati. Mradi umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili 2022/24 na utagharimu jumla ya TZS 5.1 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha miundombinu katika majengo ya Mahakama; na
ii. Kuongeza huduma za kimtandao katika ngazi zote za mahakama.

## 8.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Ofisi ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Wilaya na Shehia zilizomo katika Mikoa, kujenga mazingira mazuri ya ushiriki wa wananchi katika kudumisha amani, usalama, ulinzi wa mali zao, kuimarisha huduma za kijamii, kuhakikisha kuwa jamii inashiriki katika kupanga na kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi imepanga kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 28.0 bilioni zilizopangwa kutolewa na Serikali.

***Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama***

Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar umeanzishwa mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 ambao unagharimu jumla ya TZS 31.09 bilioni. Mradi una lengo la kuimarisha ulinzi kwa kufikia viwango vya kimataifa ili kuweka mazingira salama kwa wananchi na wageni katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2023/2024, umepangiwa kiasi cha TZS 20.0 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuweka miundombinu mipya ya mawasiliano ya ulinzi na usalama;
ii. Ununuzi wa vitendea kazi vya operesheni vya Idara Maalum za SMZ; na
iii. Kusimamia uendeshaji wa Mradi wa Mji Salama.

***Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha Zanzibar***

Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Masheha umeanzishwa mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 ambao unagharimu jumla ya TZS 15.98 bilioni. Mradi una lengo la kuimarisha Ofisi za shehia zitakazotoa huduma zinazohitajika kwa jamii, pia kuwa na mazingira bora ya kufanya kazi kwa ufanisi pamoja na kuweka nyaraka za siri za Serikali kuwa salama na kulindwa mahali sahihi. Baada ya kukamilika kwa mradi huo katika manispaa zote, mijini na maeneo ya pembezoni mwa Zanzibar itawanufaisha wananchi na kuwarahisisha kutekelezwa kazi zao kwa wepesi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2023/2024, umepangiwa kiasi cha TZS 3.0 bilioni .

***Shughuli iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza ujenzi wa majengo ya Ofisi za Masheha katika shehia 60 Unguja na Pemba.

***Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Idara Maalum za SMZ***

Mradi wa Kuimarisha Ujenzi wa Viwanda vya Idara Maalum za SMZ umeanzishwa mwaka 2022/23 - 2023/24 unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili kwa gharama ya TZS 5.72 bilioni. Mradi una lengo la kuimarisha ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo zaidi kwenye Idara Maalum za SMZ ili kuleta tija kwao na jamii kwa ujumla. Mradi unatekelezwa kwa kutumia fedha za Serikali na kwa mwaka 2023/2024, umepangiwa jumla ya TZS 5.0 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza na ujenzi wa kiwanda – Mtoni;
ii. Ununuzi wa malighafi na mashine za kuendeshea kiwanda; na
iii. Utoaji wa mafunzo ya uzalishaji wa kiwanda.

**8.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

Ofisi ina jukumu la kuimarisha huduma za usajili wa matukio ya kijamii, kutoa kumbukumbu na takwimu za jamii zilizotokana na matumizi ya mifumo ya kisasa ya usajili wa matukio ya kijamii, kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika kuchukua, kushughulikia, kuchambua, kutoa taarifa na kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya kijamii. Vile vile inashughulikia mifumo ya usajili wa taarifa za vizazi, vifo, ndoa, talaka pamoja na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo utakaogharimu kiasi cha TZS 950 milioni zinazotarajiwa kutolewa na Serikali.

***Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili***

Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili umeanzishwa mwaka 2021/22, unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 kwa gharama ya jumla ya TZS 7.0 bilioni. Mradi una lengo la kuimarisha taarifa na usalama wa mfumo wa usajili wa taarifa za matukio ya kijamii na mfumo wa vitambulisho mbali mbali. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali ambapo kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa kiasi cha TZS 950.0 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuwezesha mfumo wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi;
ii. Kufunga mifumo ya kiusalama; na
iii. Kuingiza taarifa za usajili kwenye mfumo wa usajili.

**8.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kina lengo la kuimarisha ulinzi, usalama wa raia na mali zao, kuzuia magendo ya aina zote kwa njia zinazoweza kutumika kwa kipitishia magendo, kupambana na uhalifu unaofanywa kupitia baharini ukiwemo ule wa usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya.

***Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM***

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM umeanzishwa mwaka 2016/17 na unatarajiwa kutumia jumla ya TZS 11.32 bilioni. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha wafanyakazi wa Idara Maalum za SMZ kuwa na huduma nzuri na mazingira bora ya kazi. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2023/2024, umetengewa kiasi cha TZS 2.5 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa nyumba za maafisa kambi ya Wete; na
ii. Ujenzi wa kambi ya Kizimkazi na Jengo la Ofisi - Bwefum.

**8.5.3 Kikosi cha Valantia**

Kikosi kina lengo la kutoa huduma ya ulinzi kwa kushirikiana na taasisi nyengine za ulinzi na usalama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kudumisha amani na mshikamano wa Taifa. Pia ni chombo muhimu na chenye ufanisi katika kutoa huduma ya ulinzi wa nchi, raia na mali zao.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari***

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari umeanzishwa mwaka 2017/18 unatarajiwa kutumia jumla ya TZS 10.8 bilioni. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa Idara Maalum za SMZ zinapata majengo mazuri ili kuimarisha utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wake. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee ambapo kwa mwaka 2023/2024, umetengewa kiasi cha TZS 1.5 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ukarabati wa mahanga ya kulala askari katika kambi ya Pangatupu; Ujenzi wa hanga na Ofisi kambi ya Kiashange;
ii. Ujenzi wa vibanda vya walinzi katika kambi ya Muyuni, Kikungwi, Pujini, Micheweni, Mto wa pwani, Kiashange na Mwanyanya; na
iii. Ufuatiliaji na uendelezaji wa mradi.

**8.5.4 Chuo cha Mafunzo**

Chuo kina lengo la kuwapokea wale wote wanaoletwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa Sheria, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha ili wanaporudi katika jamii wawe raia wema na watiifu. Vile vile wanaimarisha mazingira kwa kuwapatia zana za kufundishia, pamoja na kujenga uwezo kwa walimu ili kutoa huduma bora za urekebishaji na ushauri nasaha kwa wanafunzi wanapoingia na wanapotoka Chuoni hapo.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga***

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga umeanzishwa mwaka 2017/18 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25 kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umetengewa kiasi cha TZS 1.5 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya ukarabati mkubwa wa hanga la Wete-Pemba;
ii. Kujenga kituo cha afya Wete-Pemba;
iii. Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi Makao Makuu Kilimani – Unguja; na
iv. Ununuzi wa samani za Ofisi ya Wete – Pemba.

**8.5.5 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)**

JKU lina lengo la kuratibu, kusimamia na kuendesha mafunzo endelevu kwa vijana wa Zanzibar waweze kujengeka kiuzalendo, kujitegemea na kujiamini. Vile vile Jeshi linachangia kuimarisha uchumi kwa kutoa mafunzo ya uzalishaji, ufundi na kazi za amali.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU***

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU umeanzishwa mwaka 2017/18 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25 ukiwa na jumla ya

TZS 27.5 bilioni. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa Idara Maalum za SMZ zinapata majengo mazuri ili kuimarisha utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wake. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2023/2024, mradi umetengewa kiasi cha TZS 3.0 bilioni.

***Shughuli ilizopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa mbili kwa ajili ya watumishi Wawi – Pemba.

**8.5.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi**

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto na uokozi kwenye maeneo mbali mbali ya wananchi, bandarini na viwanja vya ndege Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2023/2024, Kikosi hiki kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu kiasi cha TZS 3.5 bilioni.

***Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari***

Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari umeanzishwa mwaka 2017/18 na unatarajiwa kukamilika 2024/25 ukiwa na jumla ya gharama ya TZS 8.81 bilioni. Mradi ulianzishwa kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2023/2024, umetengewa kiasi cha TZS 1.5 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa vituo na mahanga mawili maeneo ya Paje, Kiwengwa na Kibuteni kwa Unguja na Tasini kwa Pemba; na
ii. Kufanya ukarabati wa vituo na mahanga maeneo ya Marumbi na Kigunda kwa Unguja na Chanjaani kwa Pemba.

***Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto***

Mradi wa ununuzi wa magari ya zimamoto na uokozi umeanzishwa mwaka 2021/22 unatarajiwa kukamilika mwaka 2023/2024 ukiwa na jumla ya gharama TZS 4.0 bilioni. Mradi una lengo la kukabiliana na maafa yanayosababishwa na majanga ya moto kwa wananchi na mali zao, majanga yanayotokana na meli za abiria na mizigo na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na nchi kavu. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2023/2024, umetengewa kiasi cha TZS 2.0 bilioni.

*Shughuli iliyopangwa Kutekelezwa*

- Ununuzi wa gari mbili mpya za utoaji huduma ya uokozi na uzimaji moto.

**8.6 Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais**

Ofisi ina dhamana ya kuratibu na kusimamia shughuli za sekta mtambuka zikiwemo mazingira, Ukimwi, Watu Wenye Mahitaji Maalum pamoja na udhibiti wa madawa ya kulevya. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi imepanga kutekeleza miradi sita ambayo itagharimu jumla ya TZS 4.95 bilioni ambapo (TZS 3.5 bilioni kutolewa na Serikali na TZS 1.45 bilioni kutolewa na Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira***

Mradi umeanzishwa kwa lengo kutathmini hali halisi ya maeneo yaliyo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi na njia sahihi za kuhimili (Climate Change Vulnerability Assessment), pamoja na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa pwani. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka wiwili kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2023/2024. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi katika maeneo yaliyoharibika kimazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi kwa kujenga ukuta, matuta na njia za kupunguza athari pembezoni mwa fukwe (Nungwi, Msuka, Sipwese na Kisiwa Panza);
ii. Kufanya utafiti wa kina katika maeneo yote ya Zanzibar ambayo yapo hatarini kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
iii. Kusimamia na kufanya ufuatiliaji katika eneo la Sipwese; na
iv. Kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii katika eneo la Chuini.

***Mpango wa Kuirithisha Zanzibar Kijani***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha hali ya uoto wa asili wa Zanzibar na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa faida endelevu ya kimazingira, kiuchumi na kijami. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2027/28, na unagharimu jumla ya TZS 21.45 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.5 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kusaidia jamii katika shughuli za kiuchumi na za kijami Unguja na Pemba kwa kununua vifaa vya kitaaluma vya ukulima kwa Wilaya zote;
ii. Ununuzi wa mbegu na miche ya mikoko, matunda na kupanda miti kwa muda katika Wilaya zote;
iii. Ujenzi wa 'Green House' kwa kila Wilaya Unguja na Pemba;
iv. Kutoa mafunzo ya kupanda miti na kutunza mazingira kwa wakufunzi wa NGOs na viongozi wa ngazi za chini Unguja na Pemba; na
v. Kurikodi makala (documentary) juu ya mafanikio yaliyopatikana katika maeneo yaliyopandwa miti.

***Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii ya Pwani***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kujenga uwezo wa wakulima wadogo, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zitakua na matokeo yenye tija. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2021/2022 hadi 2023/2024, unagharimu jumla TZS 2.4 bilioni (USD 1,000,000). Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund) na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 774 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi na usanifu wa mabwawa ya samaki katika eneo la Mafufuni - Bumbwini kwa Unguja na Tovuni kwa Pemba;
ii. Kusaidia uanzishwaji wa vitalu vya mikoko kwa jamii katika eneo la mradi;
iii. Kuanzisha shirika la wamwagiliaji katika eneo la Bumbwini - Unguja na Tovuni - Pemba;
iv. Kuanzisha ushirika na kujenga uwezo kwa wazalishaji wa asali Unguja na Pemba; na
v. Kuendelea na ujenzi wa mashimo kwa ajili ya kuzuia maji ya chumvi kujaa katika eneo la Kiongwe kidogo.

***Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini***

Mradi una lengo la kusaidia uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa kurejesha uoto wa asili kwa kutumia mifumo ya ikolojia, kutoa elimu ya kilimo chenye kustahamili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuwajengea uwezo jamii juu ya njia mbadala za kujipatia kipato ambazo hazina athari za kimazingira. Mradi unatekelezwa kwa miaka sita, kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2023/2024, na unagharimu jumla ya TZS 1.10 bilioni. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka (United Nations Environment Programme-UNEP) na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 234 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuwawezesha wananchi kwa kuwapatia mifugo ilioboreshwa ya ngo'mbe, kuku na mbuzi pamoja na mashine za ufugaji nyuki na usindikaji katika kijiji cha Mbuyu Tende na Juga Kuu; na
ii. Kuwawezesha wananchi kwa kuwapatia mashine ya kutotolea mayai kwa utoaji wa kuku wa kienyeji katika kijiji cha Juga Kuu.

***Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Maji Machafu katika Eneo la Msingini-Kichungwani Chake Chake Pemba.***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kusafisha maji taka katika maeneo ya makaazi kwa kutumia Mfumo wa kiasili (Nature Based System) kama vile nyasi kwa ajili ya kupunguza uchafu wa mazingira hasa katika pwani ya hifadhi ya ukanda wa Pemba (PECCA). Mradi unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka (United Nations Environment Programme-UNEP) na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 192 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa chemba na mtaro wa maji machafu eneo la Peka;
ii. Ujenzi wa uzio wa kiunganishi cha mnyororo wa kuzunguka mabwawa;
iii. Ujenzi wa matuta ya udongo kwa eneo la mradi; na
iv. Kutoa mafunzo ya matumizi ya mimea katika kazi za mikono kwa wenyeji.

***Mradi wa Kuimarisha Jamii kwa Kuzingatia Ikolojia na Shughuli za Kujipatia Kipato kwa Wavuvi Wadogo Wadogo na Usimamizi wa Eneo la Hifadhi la Mkondo wa Pemba (PECCA)***

Mradi umeanzishwa kwa mpango endelevu wa matumizi ya maliasili za bahari na shughuli za kujipatia kipato kwa jamii ya eneo la Hifadhi - PECCA. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2023/2024. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 249 milioni.

***Shughuli zilizopangwa kutekelezwa***

i. Kuanzisha mfumo wa usimamizi wa taka za kaya zinazoathiri mazingira ya bahari ili kulinda mazingira ya pwani katika eneo la Tibirinzi - Chake Chake;
ii. Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi na Mpango wa Matumizi bora ya Bahari;
iii. Kuanzisha vyanzo mbadala vya kujipatia kipato ili kupunguza shindikizo la matumizi ya maliasili bahari;
iv. Kusaidia mpango wa ufuatiliaji na ufanyaji wa doria ili kudhibiti uvuvi haramu;
v. Kuandaa miongozo ya urejeshaji wa maliasili bahari;
vi. Kuanzisha maeneo ya majaribio ya biashara ya hewa ya kaboni kwenye misitu ya mikoko; na
vii. Kuandaa muongozo wa ufungaji wa shughuli za uvuvi.

**8.6.1 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya**

Mamlaka ina dhamana ya kuratibu mapambano dhidi ya biashara, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya, kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya, kutoa tiba pamoja na ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa za kulevya. Kwa mwaka 2023/2024, Tume imepanga kutekeleza mradi mmoja utakaogharimu jumla ya TZS 1.5 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya***

Mradi wa Ujenzi wa Kituo umeanza utekelezaji wake awamu ya pili (II) mwaka 2018/19 hadi 2024/2025. Mradi una lengo la kuimarisha kituo cha matibabu na kurekebisha tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Mradi unatekelezwa na Serikali pekee na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.5 bilioni.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuendelea na ujenzi wa jengo kuu la utawala katika kituo cha Kidimni;
ii. Kuendelea na ujenzi wa jengo kuu la soba liliopo Kidimni;
iii. Kuendelea na ujenzi wa kibanda cha mlinzi Kidimni;
iv. Ukarabati wa jengo la Ofisi za Mamlaka iliopo Kilimani; na
v. Kuanza na ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia Kangagani – Pemba.

### 8.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sambamba na kusimamia shughuli za Muungano kwa kufuata misingi ya katiba na sheria pamoja na kulinda haki za binadamu na ushirikishwaji. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja itakayogharimu jumla ya TZS 17.6 bilioni (TZS 100 milioni kutolewa na Serikali na TZS 17.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

*Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (TASAF III) Kipindi cha Pili*

Programu inatekelezwa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, inagharimu jumla ya TZS 112.2 bilioni. Programu imeanza utekelezaji kwa awamu (III) mwaka 2020/21 na kumalizika ifikapo mwaka 2024/25, ikiwa na lengo la kuziwezesha kaya masikini sana kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu ya kibinadamu hasa chakula, afya na elimu. Programu hii inakusudia kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wananchi katika nyanja mbali mbali za elimu, afya na ajira za muda, kwa lengo la kuwawezesha wananchi ili waweze kujikwamua na umasikini. Kwa mwaka 2023/2024 programu hii imepangiwa kiasi cha TZS 17.6 bilioni ambazo TZS 100 milioni kutoka Serikalini na TZS 17.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali*

i. Kuratibu shughuli za TASAF baina ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara;
ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mradi wa TASAF; na
iii. Kuandaa mikutano ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Wataalamu.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuanza ujenzi wa kituo cha mama na mtoto katika eneo la Upenja Unguja;
ii. Kuanza ujenzi wa ukumbi wa kufanyia mitihani skuli ya Bambi - Unguja;
iii. Ukarabati wa skuli na ukumbi wa kufanyia mitihani katika skuli ya Kizimkazi Mkunguni - Unguja; na
iv. Uhaulishaji wa fedha kwa kaya masikini (walengwa wa mradi).

**8.8 Wizara ya Afya**

Wizara ya Afya ina jukumu na wajibu wa kusimamia afya za wananchi wote wa Zanzibar ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi wa Taifa na kuleta maendeleo endelevu. Sekta hii inatekeleza Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) kwa kuimarisha miundombinu na mifumo ya utowaji wa huduma za afya kwa kuimarisha uwezo wa sekta katika utoaji wa huduma za afya zilizobora kwa wananchi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Afya imepanga kutekeleza programu saba na miradi minne ya maendeleo yenye thamani ya jumla ya TZS 76.80 bilioni (TZS 54.18 bilioni kutoka Serikalini na TZS 22.62 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo).

***Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi***

Programu hii imeanza mwaka 2023/2024 na ina lengo la kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya ya msingi ili viweze kutoa huduma za afya ya msingi zenye kiwango na kuimarisha afya ya jamii. Programu hii inatekelezwa na Serikali ambapo kwa mwaka 2023/2024 imepangiwa jumla ya TZS. 20.0 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Kuvifanyia ukarabati vituo vya afya 18; na
ii) Kuvijenga tena vituo vya afya 25 ambavyo havijafikia vigezo vinavyohitajika.

***Programu ya Kuimarisha Huduma za Mama na Mtoto***

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za mama na mtoto nchini. Programu imeanza mwaka 2022/23 na inatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano kwa gharama ya USD 25 milioni. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Kujenga miundombinu ya usafi wa mazingira (WASH) katika vituo vya Afya vya Miwani, Shungi na Finya;
ii) Kuifanyia Mapitio Mitaala ya Uuguzi na Ukunga;
iii) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wataalamu wa afya kwa ngazi ya Shahada ya Uzamili;
iv) Kuwajengea uwezo wahudumu wa afya wa kujitolea wawe na uelewa zaidi wa masuala ya lishe, huduma za mama na mtoto na usafi wa mazingira; na
v) Ununuzi wa kompyuta ili kuimarisha huduma za kidijitali katika vituo vya afya.

***Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa***

Programu ina lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili wawe na utulivu wa kufanya kazi na kuongeza ufanisi na kupatikana muda wote itakapotokea dharura. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya TZS 20.0 bilioni zimetengwa kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mkoa –Lumumba;
ii. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya – Pangatupu;
iii. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya - Mwera Pongwe;
iv. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya – Kitogani;
v. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya – Vitongoji; na
vi. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya – Kinyasini.

***Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya***

Program hii ina lengo la kuimarisha miundombinu itakayosaidia katika utoaji wa huduma za afya zenye ubora na viwango vinavyokubalika. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Kuanza ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa – Unguja;
ii) Kuanza ujenzi wa Maabara ya Bio-chemistry; na
iii) Kufanya malipo kwa fedha zilizosalia kwa Wakandarasi (retention).

***Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Afya***

Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Afya umeanza mwaka 2023/2024 una lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma bora za afya. Utekelezaji wa mradi huu utajumuisha hospitali za Wilaya na Mkoa Unguja na Pemba. Aidha, mradi huu utatekelezwa kwenye vituo vya afya ya msingi (Dispensaries na Health Centers) ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kutoa huduma kidigitali (Digital Health Transformation). Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya TZS 10.0 bilioni zimepangwa kutoka Serikalini kutekeleza shughuli za mradi.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Utandazaji wa Mkonga wa Taifa kwenye vituo vyote 168 vya afya ya msingi;
ii) Ufungaji wa Mtandao wa ndani (LAN) kwenye Vituo 168;
iii) Ununuzi wa vifaa vikiwemo kompyuta, UPS, Printer na Laptops; na
iv) Kuendesha mafunzo ya mifumo kwa watumiaji.

***Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar***

Programu hii ina lengo la kutokomeza maradhi ya malaria kwa kuhakikisha kwamba maradhi haya yanamalizika kabisa hapa Zanzibar. Aidha, programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 1.53 bilioni (TZS 550.0 milioni kutoka Serikalini na TZS 977.7 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya utekelezaji.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i) Uchunguzi na utibabu wa ugonjwa wa malaria; na
ii) Udhibiti wa mbu waenezao malaria.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i) Uchunguzi na utibabu wa ugonjwa wa malaria;
ii) Ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria; na
iii) Udhibiti wa mbu waenezao malaria.

***Programu Shirikishi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma***

Programu hii ina lengo la kupambana na maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma. Lengo kuu ni kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kupunguza vifo vitokanavyo na maradhi ya kifua kikuu, homa ya Ini na kupunguza maambukizi ya ukoma. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Jumla ya TZS 1.55 bilioni zimetengwa kutekeleza mradi huu (TZS 1.05 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS. 500.0 milioni kutoka Serikalini) kwa mwaka 2023/2024.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za kinga na tiba ya Homa ya Ini; na
ii. Kuimarisha utoaji wa huduma za UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanoishi na virusi vya UKIMWI; na
ii Kuimarisha huduma ya utoaji wa kinga ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

***Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto (IRCH)***

Programu hii ina lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Jumla ya TZS 5.8 bilioni zimetengwa kwa programu hii (TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa mwaka 2023/2024.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya miaka 5 na watoto wachanga;
ii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na kupunguza vifo vya mama na mtoto;
iii. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za mama na mtoto; na
iv. Kuimarisha huduma za damu salama.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya umri wa miaka 5 na watoto wachanga;
ii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo na vifo vya mama na mtoto; na
iii. Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo za mama na watoto.

***Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya-Kizimkazi***

Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024 na unalengo la kuimarisha miundombinu ya afya kwa kujenga kituo cha afya ambacho kitatoa huduma bora kwa wananchi wa eneo hilo na maeneo jirani. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo jumla ya TZS. 4.0 bilioni zimetenga kwa mwaka 2023/2024.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Ujenzi wa Kituo cha Afya; na
ii) Ununuzi wa vifaa tiba.

***Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja***

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma katika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma nzuri na zenye kukidhi mahitaji. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 10.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kumlipa Mshauri Elekezi;
ii. Kufanya ukarabati wa majengo ya hospitali ya Mnazi Mmoja; na
iii. Uratibu na usimamizi wa mradi.

***Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja***

Mradi huu unalengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Mradi huu unatekelezwa na Serikali na kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, umetengewa TZS 1.1 bilioni.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i) Ununuzi wa machine na vifaa tiba;
ii) Ununuzi wa mtambo wa kuchomea taka tiba (incinerator); na
iii) Ununuzi wa samani.

**8.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi**

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kusimamia upangaji wa matumizi bora na upatikanaji wa rasilimali ardhi kupitia program mbalimbali za urasimishaji. Mipango mizuri ya ardhi itasadia kugawanya matumzi ya ardhi kulingana na shughuli mbalimbali zinazoendelea kutekelezwa nchini, ikiwemo uwekezaji, michezo, biashara, viwanda, kilimo na makaazi. Aidha, Wizara ina jukumu la kuratibu sekta ya makaazi ambayo ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora na salama kwa wananchi. Wizara hutumia wadau mbalimbali wakiwemo Shirika la Nyumba, Mabenki na Mifuko ya hifadhi ya jamii ili kurahishsiha upatikanaji wa makaazi yaliyobora, na ya kisasa. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara hii imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo kupitia Kamisheni ya Ardhi.

***Mradi wa Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi***

Mradi huu ulianza mwaka 2022/23 ukiwa na lengo la kuipanga ardhi yote ya Zanzibar ili kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi, ikiwemo changamoto ya usambazaji wa huduma za jamii, uwekezaji, miundombinu, mahitaji ya makaazi, viwanda pamoja na maeneo ya wazi. Aidha, mradi utasaidia kupunguza changamoto ambazo hujitokeza katika maeneo ya uwekezaji haswa katika maeneo ya fukwe. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 4.5 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kutayarisha mipango ya maendeleo ya usimamizi wa miji pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti;
ii. Ununuzi wa vitendea kazi katika utekelezaji wa mpango wa matumzi ya ardhi;
iii. Kutayarisha mipango ya maendeleo kwa vijiji ambavyo vipo karibu na EPZ;
iv. Uimarishaji wa Miji na upangaji wa maeneo ya nje ya Miji;
v. Kutayarisha mipango ya maendeleo na usimamizi wa NESAP; na
vi. Kuimarisha maeneo ya wazi.

## 8.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kukuza na kuendeleza sekta ya biashara na viwanda kwa lengo la kuleta maendeleo nchini. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara hii itatekeleza shughuli za maendeleo kupitia miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 28.4 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Park)***

Mradi huu umeanza mwaka 2019/20 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26, Mradi una lengo la kuvutia uwekezaji, kutengeneza ajira na kuongeza mauzo ya nje kwa kukabiliana na vikwazo vinavyozuia michakato ya ukuaji wa viwanda Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mradi huu umepangiwa jumla ya TZS bilioni 26.0 kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan) na kufanya utafiti wa eneo (Topograpyical and Geotropical Survey) kwa eneo la uwekezaji Pangatupu;
ii. Kujenga mnara na tangi la maji la lita 7,000 katika eneo la uwekezaji Chamanangwe;
iii. Kujenga ukuta wa uzio, mabanda matatu ya viwanda na barabara za ndani katika eneo la uwekezaji Chamanangwe; na
iv. Kujenga ukuta wa uzio, mabanda matano ya viwanda pamoja na miundombinu ya umeme na TEHAMA katika eneo la uwekezaji Dunga.

***Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar***

Mradi huu ulianza mwaka 2017/18 na kutarajia kukamilika mwaka 2024/25 ambapo lengo kuu ni kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa kuweka miundombinu ya huduma bora za kibiashara na kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.4 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya umeme na maji;
ii. Kuweka sawa (Leveling) eneo la maonesho na kujenga ukuta;
iii. Ununuzi wa vifaa vya maonesho ikiwemo mashamiana na zana zake; na
iv. Ujenzi wa vibaraza vya kuwekea mashamiana, vyoo, maegesho ya vyombo vya moto pamoja na ufungaji wa vifaa vya ulinzi katika Uwanja wa Maonesho.

**8.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali**

Maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika taifa lolote yanapatikana kwa kuwepo kwa misingi imara ya Elimu inayoenda sambamba na mabadiliko ya kisayani na teknolojia. Serikali imekuwa ikijidhatiti kuboresha miundombinu ya elimu kwa lengo la kuwa na mazingira bora ya utoaji wa elimu itakayoimarisha rasilimali watu ili kukidhi mahitaji ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Mpango wa Maendeleeo wa Zanzibar wa 2021-2026. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepangiwa jumla ya TZS 181.07 bilioni ambapo Serikali imepanga kutoa TZS 98.97 bilioni na Washirika wa Maendeleo TZS 82.10 bilioni ili kutekeleza Programu moja na Miradi minne ya Maendeleo.

***Programu ya Uimarishaji Miundombinu ya Elimu***

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuinua ubora wa elimu kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza. Kwa mwaka 2023/2024 Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 131.23 bilioni (TZS 59.04 bilioni kutoka Serikalini na TZS 72.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kutekeleza kazi zilizopangwa kutekelezwa.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Mchango wa Serikali katika ujenzi wa vituo vitano vya Mafunzo ya Amali, Chuo cha Ubaharia na jengo la mafunzo ya mafuta na gesi na kituo cha kuwaendeleza wajasiriamali;
ii. Ujenzi wa nyumba 20 za walimu;
iii. Kujenga skuli 31 za ghorofa zikiwemo 12 za msingi na 19 za Sekondari; na
iv. Mchango wa Serikali katika ujenzi wa dakhalia katika Skuli za Paje Mtule na Chwaka Tumbe.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ujenzi wa Majengo Matano ya Ofisi katika Wilaya (Kaskazini A, Magharibi B, Kusini, Micheweni na Chake Chake) zenye maktaba, Ofisi za ukaguzi wa elimu na chumba cha TEHAMA Unguja na Pemba na kukamilisha Ofisi ya Wilaya ya Elimu ya Mkoani pamoja na kuzipatia vifaa;
ii. Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu Kiuyu na Mazizini, TC Kiembesamaki na Maktaba Kuu;

iii. Ujenzi wa vituo vitano vya Mafunzo ya Amali, Chuo cha Ubaharia na jengo la mafunzo ya mafuta na gesi na kituo cha kuwaendeleza wajasiriamali;
iv. Ukarabati wa Skuli 23 za Maandalizi, Msingi na Sekondari zikiwemo Kidongochekundu, Chanjamjawiri, Muyuni Sekondari, Chumbuni Msingi, Faraja Sekondari, Kengeja-Dakhalia Sekondari, Kiuyu Minungwini, Chutama, Mikunguni, Fidel Castro Ukumbi, Dakhalia ya watoto wa Kiume Lumumba, Maungani, Uzini Msingi, Chaani Sekondari, Jang'ombe Maandalizi, Kizimbani Msingi, Mahonda, Ndagoni Msingi, Ole, Maziwa Ng'ombe na Mahonda;
v. Kukiimarisha Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia kwa kutanua na kufanya ukarabati wa maabara na karakana;
vi. Kujenga jengo la Ofisi la Wizara Unguja na Pemba;
vii. Kujenga madarasa 12 mapya ya msingi katika maeneo ya Kisakasaka (8) na Umbuji (4);
viii. Kujenga vyoo 60 katika skuli za msingi na sekondari;
ix. Ujenzi wa dakhalia katika skuli za Paje Mtule na Chwaka Tumbe; na
x. Kusaidia ujenzi wa skuli ya ghorofa ya Mtambile iliyoanzishwa na wananchi.

***Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha watoto wote waliofikia umri wa kuanza skuli kwa ngazi ya maandalizi na msingi wana mazingira mazuri ya kupata elimu bora. Kwa mwaka 2023/2024 mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 6.12 bilioni (TZS 4.62 ni Ruzuku na TZS 1.50 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuzipatia skuli vikalio zikiwemo skuli mbili za elimu mjumuisho Unguja na Pemba (makabati 40 (4 in 1), vitanda 160 na magodoro 160);
ii. Kuimarisha elimu ya msingi katika kusoma, kuandika na kuhesabu kwa darasa la kwanza hadi la nne;
iii. Kuimarisha vituo vya Habari na Mawasiliano ya Elimu;
iv. Kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya Mitaala Mipya; na
v. Kutoa mafunzo kwa walimu wa maandalizi na msingi kupitia mtaala mpya.

***Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima***

Mradi huu una lengo la kuhakikisha kila mtoto anapatiwa haki yake ya kupata elimu katika ngazi ya sekondari ya lazima. Kwa mwaka 2023/2024 mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 17.35 bilioni (TZS 15.17 bilioni kutoka Serikalini na TZS 2.18 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Ununuzi wa samani.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo***

i. Kuzipatia skuli 21 Kompyuta 1,500 (Kompyuta 32 kwa skuli) na Kompyuta 70 kwa wafanyakazi wa Wizara Unguja na Pemba;
ii. Kuimarisha mfumo wa Rasilimali Watu wa Wizara; na
iii. Kuwapatia walimu mafunzo ya ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza na Mafunzo ya Uongozi wa skuli kwa walimu wakuu.

***Mradi wa Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali***

Lengo la mradi huu ni kutoa elimu ya amali ili kupunguza utegemezi wa ajira Serikalini na kuwa na wataalamu wazalendo katika fani mbali mbali. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.76 kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuvipatia vyuo vya Amali vifaa vya kisasa ili viweze kutoa mafunzo ya vitendo.

***Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuongeza Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu kwa kuwapatia mikopo na kuimarisha miundombinu ya vyuo vikuu. Kwa mwaka 2023/2024 mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 21.60 bilioni (TZS 20.00 bilioni kutota Serikalini na TZS 1.60 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) ili kutekeleza kazi zilizopangwa.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Kuwapatia mikopo wanafunzi wanaojiunga na masomo katika vyuo vya elimu ya juu

*Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo*

- Kuwapatia mafunzo wahadhiri wa KIST katika matumizi ya maabara na karakana.

**8.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**

Lengo kuu la Wizara ni kusimamia sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili kuweza kuimarisha na kuendeleza maeneo hayo na kutatua changamoto zilizopo. Pia, Wizara ina jukumu la kuhakikisha habari zinatolewa na kupokelewa kwa usahihi na kwa wakati, kuwawezesha vijana na kuwatafutia fursa mbali mbali za ajira, kudumisha utamaduni na kuimarisha michezo kwa lengo la kuimarisha afya za wananchi na kuongeza ajira. Kwa mwaka wa 2023/2024, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inatarajia kutekeleza programu moja itakayogharimu kiasi cha TZS 34.28 bilioni.

***Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo***

Lengo la mradi huu ni kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Mradi huu umeanza 2021/22 hadi 2025/26, kwa mwaka 2023/2024 mradi unatarajiwa kutumia jumla ya TZS 34.28 bilioni ambapo TZS 33.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.28 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali*

i. Ukarabati wa uwanja wa Amani na Mao Ze Dong; na
ii. Ujenzi wa viwanja vya Wilaya Unguja na Pemba.

*Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa na Washirika wa Maendeleo*

- Ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya vinne (6 in 1).

**8.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo**

Wizara imehusisha sekta muhimu katika ukuzaji uchumi kwa kutoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kupambana na umasikini kwa kuwapatia chakula, ajira pamoja na kuimarisha huduma za kilimo. Aidha, Wizara ina jukumu la kusaidia upatikanaji wa mbegu na utoaji wa mafunzo kwa wakulima na wafugaji. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo, ambapo zitagharimu jumla ya TZS 68.52 bilioni (TZS 25.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 43.52 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Programu ya Umwagiliaji (Awamu ya II)***

Programu imeanzishwa kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga, kuwawezesha wakulima kwa kuwajengea uwezo wa uzalishaji kwa kutumia pembejeo za kilimo. Programu hii itagharimu jumla ya kiasi cha TZS 40.0 bilioni hadi kukamilika kwake na kwa mwaka 2023/2024, inatarajiwa kutumia jumla ya TZS 31.70 bilioni ambapo (TZS 500 milioni kutoka Serikalini na TZS 31.20 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo***

i. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 300 katika bonde la Cheju B;
ii. Uungaji wa umeme mkubwa kwenye visima vya umwagiliaji maji kwenye bonde la Cheju B;
iii. Ujengaji wa misingi ya ndani (tertial canals) kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani na Mlemele;
iv. Kusimamia maeneo yaliyokwisha kujengwa miundombinu mipya ya umwagiliaji maji yenye ukubwa wa hekta 1,053 ikiwemo kuwapa mafunzo ya taaluma juu ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa kamati na wakulima viongozi;
v. Ukamilishaji na utatuaji wa changamoto ya uvujaji maji katika bwawa la Chaani; na
vi. Ukamilishaji wa uungaji wa bomba za maji kwenye visima katika bonde la Kilombero.

***Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo***

Programu ina lengo la kuimarisha na kuinua sekta ya kilimo na mifugo kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo nchini. Kwa mwaka 2023/2024 programu hii itajumuisha miradi mitatu itakayogharimu jumla ya TZS 4.8 bilioni ambapo (TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 2.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya mifugo ili kuongeza kasi ya uzalishaji na usalama wa mifugo inapoingia nchini pamoja na mazingira bora ya uchinjaji wa mifugo. Mradi huu unagharimu kiasi cha TZS 11.2 bilioni kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2023/2024. Kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ukarabati wa eneo la karantini ya mifugo katika maeneo ya Kisakasaka - Unguja;
ii. Ununuzi wa mtambo wa kuzalisha gesi ya naitrojeni (liquid nitrogen) kwa ajili ya kuhifadhia mbegu za kupandisha ng'ombe kwa sindano;
iii. Ujenzi wa miundombinu ya karantini ya mifugo katika eneo la Gando Nziwengi; na
iv. Ujenzi wa miundombinu ya Maabara ya Utafiti wa Mifugo Unguja na Pemba;

***Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)***

Mradi huu unatekelezwa kisiwani Pemba, kwa lengo la kuimarisha mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika ukuaji wa uchumi shirikishi nchini Tanzania pamoja na kuiwezesha asali bora inayozalishwa kwa njia endelevu ya mazingira ya kupenya katika masoko. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 514 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki juu ya mbinu mpya za ufugaji nyuki na uzalishaji bora, kutambua aina za nyuki pamoja na mazao mengine ambayo yanapatikana kutokana na nyuki nchini Tanzania bara;
ii. Uanzishwaji na uendelezaji wa mashamba ya wafugaji nyuki (manzuki) Pemba; na
iii. Kuwaunganisha wazalishaji wa mazao ya nyuki na masoko.

***Mradi wa Kilimo Tija***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuendeleza fursa za kiuchumi na kuimarisha mifumo ya masoko kwa mazao ya mboga na matunda, hasa kwa vijana ili

kuongeza fursa za ajira na ujasiriamali, pamoja na kuongeza upatikanaji wa teknolojia za kilimo zinazoimarisha uzalishaji wa kilimo cha kibiashara na unaozingatia mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 2.3 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kusaidia shughuli za ugani ili kuweza kufikisha huduma bora za ugani kwa wakulima kwa kuimarisha uwezo wa mabwana shamba pamoja na kushajihisha wadau zaidi wa ugani;
ii. Kuanzisha kanzidata ya wakulima itakayoimarisha ukusanyaji wa taarifa, ukaguzi na kusaidia mipango ya Wizara;
iii. Kuimarisha mabaraza ya vijana katika ngazi ya Wilaya ili kuwajenga uwezo katika uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na kuendeleza biashara katika minyororo ya thamani;
iv. Kuisaidia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI kuandaa benki ya hifadhi ya mimea kwa mazao ya mboga na matunda yenye asili ya Afrika na kuanzisha vitalu kwa ajili ya kufanyia majaribio na usambazaji wa matokeo mbegu bora za mimea; na
v. Kushirikiana na sekta binafsi katika kuandaa ramani ya udongo ya Zanzibar na kuwawezesha wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kufikia mitaji itakayosaidia biashara zao;

***Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao***

Programu imeanzishwa kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo ili kuongeza upatikanaji wa chakula kwa wakulima na wananchi nchini. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 9.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Mradi wa Kupambana na Sumu Kuvu Tanzania (TANIPAC)***

Mradi una lengo la kupuguza athari zinazotokana na sumukuvu katika mahindi na njugu nyasa kwa kutoa taaluma na kuimarisha miundombinu na teknolojia kabla na baada ya mavuno. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara utekelezaji wake ni kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2019/2020 hadi 2023/2024. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 485 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutoa mafunzo ya udhibiti wa sumukuvu kwa wadau wa mnyororo wa thamani kwa wakulima wa mazao ya mahindi na njugu nyasa; na
ii. Kutoa mafunzo ya utengenezaji wa vizimba vya chuma kwa vijana 40 Unguja na Pemba na utoaji wa teknolojia ya darasa za kukaushia.

***Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa chakula kwa wakulima na wananchi wa Zanzibar. Mradi unajumuisha uwezeshaji kwa wakulima ili kupata masoko baada ya mavuno kwa kuongeza thamani na kipato kwa mazao ya kilimo. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2025/26 na utagharimu jumla ya TZS 10.07 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 421 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa vifaa vya kuimarisha mfumo wa uingizaji na utoaji wa mazao, kukusanyia sampuli za wadudu wa matunda, kwa ajili ya kampeni ya nzi wa matunda na vifaa vya maabara ya karantini;
ii. Kufanya upembuzi yakinifu juu ya matumizi ya mbinu mchanganyiko katika maeneo maalum; na
iii. Kukusanya takwimu za matunda kwa utaratibu maalum (systematic fruit sampling).

***Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (AGRICONNECT)***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kusaidia sera bora za mazingira wezeshi na uwekezaji zaidi wa sekta binafsi, kukuza minyonyoro ya thamani kwa kuboresha uzalishaji, usindikaji, uuzaji na kuwaunganisha wakulima na masoko. Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2023/2024. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 8.6 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuwajengea uwezo wakulima 10,500 (wanawake na vijana) ili kuweza kupata na kutumia vyakula vyenye lishe bora pamoja na wakulima na utaalamu wa viwango endelevu vya hiari (VSS) Unguja na Pemba;

ii. Kuongeza thamani kwa kujenga majengo mawili ya kusindika mazao, kushughulikia masoko na kilimo biashara;
iii. Kuwasaidia wakulima wadogo wadogo 1,767 kwa kuwasogezea huduma za fedha na kuendeleza uzalishaji wa mazao ya mboga, viungo na matunda ili kuongeza kipato chao;
iv. Kuwapatia mitaji wajasiriamali na wakulima wadogo kwa vikundi 45 ili kuendeleza miradi ya kilimo cha "horticulture" pamoja na usindikaji;
v. Kufanya utafiti wa kudhibiti viumbe waharibifu wa mazao pamoja na kuchunguza mabaki ya madawa ya mimea katika mazao; na
vi. Kuendeleza mpango wa kusambaza taarifa za masoko na elimu kwa wadau wa mazao ya bustani.

***Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha haki ya upatikanaji wa chakula katika ngazi ya kaya na Taifa unafanikiwa, kwa ukarabati wa maghala na ununuzi wa chakula. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 22.5 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa vituo vitatu vya kuhifadhia chakula (nafaka) viwili kwa Unguja na moja Pemba;
ii. Ujenzi wa hifadhi na mitambo ya baridi miwili katika bandari ya Mkoani Pemba na Unguja;
iii. Ukarabati wa maghala sita Pemba (Dodeni, Weni na Pujini) na Unguja (Cheju, Kilombero na Donge Muanda);
iv. Ununuzi wa vinu vitatu vya kukobolea mpunga (kimoja Pemba na viwili Unguja);
v. Ununuzi wa tani 100,000 za mpunga na tani 300,000 za mahindi; na
vi. Ununuzi wa magari matatu na malori matatu kwa ajili ya shughuli za hifadhi ya chakula.

## 8.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii, wazee na watoto ili kuwa na hali bora za kimaisha. Aidha, Sekta hii imeundwa kwa lengo la kushughulikia maendeleo ya kijamii na kuleta usawa wa kijinsia. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Sekta hii

imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo utakaogharimu kiasi cha TZS 2.14 bilioni.

***Mradi wa Hifadhi ya Wazee***

Serikali imeanzisha mradi huu kwa lengo la kuimarisha hali za wazee kwa kuimarisha makaazi yao, usalama na upatikanaji wa huduma za msingi kikamilifu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.1 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 1.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 636 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya ukarabati katika makaazi ya wazee yaliopo Limbani - Pemba na Sebleni - Unguja;
ii. Ununuzi wa vifaa na thamani; na
iii. Uratibu wa shughuli za mradi.

## 8.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wizara ya Maji, Nishati na Madini inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni maji, nishati na madini. Wizara hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote zilizo chini ya sekta hizo ili kuweza kuhakikisha wakaazi wa Zanzibar wanafaidika na huduma za maji safi na salama, upatikanaji na usambazaji wa nishati endelevu kwa ufanisi na unafuu. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza jumla ya programu mbili zitazogharimu kiasi cha TZS 110.66 bilioni. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 48.71 bilioni kutoka Serikalini na TZS 61.95 bilioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar***

Programu hii ina lengo la kusimamia na kuhakikisha huduma za usambazaji maji safi na salama zinapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi wote kunufaika na huduma hiyo muhimu katika jamii. Kwa mwaka 2023/2024, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 77.51 bilioni (TZS 24.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 53.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kutekeleza shughuli zake kupitia miradi saba ya maendeleo kama ifuatavyo:-

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi***

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi una lengo la kuongeza uzalishaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi ili kutosheleza mahitaji kwa wananchi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka 2023/2024 na kwa mwaka 2023/2024, jumla ya TZS 9.96 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimepangwa kutumika.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya mapitio ya taarifa zilizopo na makadirio ya mahitaji ya maji;
ii. Kufanya utafiti wa hali ya mazingira (EIA) pamoja na utafiti wa maeneo yatakayopita mradi;
iii. Kufanya mapitio ya tarifa zilizopo na makadirio ya mahitaji ya maji; na
iv. Kuendelea na hatua za awali za matayarisho ya mradi.

***Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)***

Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) unalenga kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji safi na salama katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi A, (Mfenesini, Masingini na Kizimbani) Magharibi B (Dimani na Kidutani) na Wilaya ya Kati (Jumbi- Mkorogo) pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kuwa tatizo la maji katika maeneo yaliyokusudiwa linaondoka kabisa na wananchi wanaweza kupata maji safi na salama muda wote. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya India. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 29.66 bilioni (TZS 11.16 bilioni kutoka Serikalini na TZS 18.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ulipaji wa fidia za vipando na majengo katika maeneo ya Mkorogo, Dimani, Maungani, Mfenesini, Dole, Kidutani na Masingini; na
ii. Kuratibu vikao vya Kamati Kiongozi na Kamati ya Wataalamu.

***Shughuli Iilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo***

- Malipo kwa ajili ya Uangalizi wa Mradi (Deffect Liability Period)

***Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar***

Mradi umeanzishwa kwa lengo kuu la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Zanzibar Utekelezaji wa shughuli za mradi huu utadhaminiwa na Washirika wa Maendeleo kwa gharama ya TZS 80.5 bilioni ambapo kwa upande wa Serikali utatakiwa kugharamia malipo ya fidia kwa maeneo yatakayoathirika na mradi pamoja na kazi za uratibu wa shughuli za mradi ikiwemo ufuatiliaji na tathmini. Kwa mwaka 2023/2024, jumla ya TZS 14.23 bilioni (2.85 bilioni kutoka Serikalini na 11.38 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepangwa kutumika.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ulipaji wa fidia kwa maeneo yatakayoathirika na mradi; na
ii. Uendeshaji wa shughuli za mradi.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo***

- Malipo ya awali ya Mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi.

***Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar***

Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar una lengo kuendeleza na kuimarisha huduma ya maji safi na salama Zanzibar kwa maeneo ya Kizimbani No. 2, Jendele- Chwaka, Banda Maji, Donge, Miwani, Ndijani -Muembe Punda, Ubago - Nyakurungwi, Dunga jumba la mawe, Mwera- Pongwe, Chaani -Kikobweni, Mkataleni – Msufini, Mchangani-Mkiwa, Pangeni, Machui kwa Bavuai, Upenja, Kitope- Skuli na Mkokotoni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa TZS 10.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa mabomba na viungio (Pipe Fittings);
ii. Uchimbaji msingi na ulazaji bomba;
iii. Ujenzi wa vibanda, uzio na uwekaji umeme;
iv. Ununuzi na ufungaji pampu; na
v. Ununuzi wa mita za maji (Smart meter).

***Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar***

Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar una lengo la kufanya utafiti kiwango cha maji kilichopo ardhini Unguja na Pemba. Utafiti huo utaiwezasha Serikali kugundua kiwango cha rasilimali maji kilichoko chini ya ardhi ili kurahisisha na kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi mijini na vijijini. Mradi huu unatekelezwa kwa msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024, jumla ya TZS 2.60 bilioni zimepangwa kutumika.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kufanya upembuzi yakinifu juu ya kujua kiwango cha maji kilichopo ardhini katika visiwa vya Unguja na Pemba.

***Mradi wa Usimamizi wa Maji***

Mradi wa Usimamizi wa Maji lengo la kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa afya za wananchi kwa kufanya ununuzi wa chlorine, kusimamia na kuangalia ubora wa maji Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2023/2024 mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 75.0 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Utibabu wa maji kwa usimamizi na uangalizi wa ubora wa maji.

***Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar***

Programu ina lengo la kuimarisha huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi kupata huduma hiyo kwa uhakika zaidi. Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 33.14 bilioni (TZS 24.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na imepanga kutekeleza miradi mitatu ifuatayo:-

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme***

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma za umeme katika vijiji 305 (180 Unguja na 125 Pemba) ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma salama na ya uhakika. Mradi huu ni wa miaka minne (2021-2025) na unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 162.75 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 17.0 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Usambazaji wa umeme katika vijiji vya Unguja na Pemba;
ii. Ununuzi na nguzo na vifaa vya umeme; na
iii. Uvutaji wa njia mpya za umeme.

***Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)***

Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka sita (2022-2027) na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 372.48 bilioni kwa lengo la kuimarisha utekelezaji katika sekta ya nishati kwa kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.08 bilioni (TZS 7.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.88 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo***

i. Ujenzi wa laini kubwa ya umeme wenye uwezo wa kilovoti 132 pamoja na kufanya malipo kwa Mshauri Elekezi;
ii. Uwekeaji wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi na undelezaji wa miundombinu ya umeme; na
iii. Kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme wa jua.

***Mradi wa Nishati Jumuishi Zanzibar (Zanzibar Energy Consolidation)***

Mradi wa Nishati Jumuishi Zanzibar umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha wa huduma ya umeme ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya umeme iliyo salama na ya uhakika. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 67.63 milioni.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Ufungaji wa mita janja (smart meters) pamoja na kuunganisha mifumo ya malipo.

## 8.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Lengo kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kukuza uchumi wa Zanzibar kwa kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha wajasiriamali ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya biashara na viwanda ambayo itasaidia upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana kupitia Uchumi wa Buluu. Wizara hii inasimamia na kuendeleza masuala yote yanayohusiana na uchumi wa buluu Zanzibar ikiwemo utekelezaji wa shughuli za uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha bahari, ufugaji wa mazao baharini, utalii wa baharini na fukwe, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia sambamba na uratibu wa utawala na mazingira ya baharini. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza jumla ya programu mbili na miradi 12 ya maendeleo ambayo imepangiwa jumla ya TZS 71.75 bilioni (TZS 35.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 36.25 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi***

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi imeanzishwa kwa lengo la kuongeza tija endelevu, uthabiti, faida na biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. Programu imeanza mwaka 2021/22 ni ya miaka mitano (2021-2026) ambayo inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kutumia fedha za Washirika wa Maendeleo pekee. Kwa mwaka 2023/2024, program hii imepangiwa kiasi cha TZS 11.92 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha uvuvi wa ubia na sekta binafsi kwa kununua meli 2 za uvuvi, kutayarisha mfumo wa uvuvi wa kibiashara na mfumo wa ubia;
ii. Kufanya uchambuzi yakinifu wa uendeshaji wa uvuvi wa ubia;
iii. Ujenzi wa kiwanda kimoja mjumuishi cha uchakataji wa samaki pamoja na mitambo baridi ya kuhifadhia samaki;
iv. Ununuzi wa lori la jokofu la tani 10 kwa ajili ya matumizi ya kampuni ya ZAFICO;
v. Kusaidia miundombinu ya vituo viwili vya mafunzo ya uvuvi na ufugaji wa viumbe bahari vitakavyojengwa Unguja na Pemba;
vi. Ujenzi wa kituo cha kupokelea na kulelea vifaranga vya samaki pamoja na kitalu Pemba;

vii. Ujenzi wa maabara moja ya uzalishaji wa mbegu bora za mwani pamoja na vitalu 41 vya uzalishaji wa mbegu bora za mwani pamoja na kuwajengea uwezo wakulima;
viii. Kufanya utafiti wa uzalishaji na ukuzaji wa aina tatu za samaki ambao ni majongoo bahari, kaa na "milk fish";
ix. Kufanya upembuzi wa shughuli za kilimo cha mwani na ufugaji wa samaki katika maeneo ya hifadhi na kuwapatia vifaa na utaalamu wakulima wa mwani na wafugaji wa samaki;
x. Kukuza usarifu wa mazao kwa kujenga makaushio yanaotumia jua kwa dagaa na mwani pamoja na kununua mtambo wa kusarifu mwani; na
xi. Kuratibu shughuli za utekelezaji wa mradi ikiwemo kufanya uchambuzi wa awali, ununuzi wa vyombo vya usafiri, ufuatiliaji na tathmini.

***Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia***

Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia ya juu na chini (Upstream and Downstream) imeanza mwaka 2022/23 na inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2022-2027) kwa gharama ya jumla ya TZS 173.36 bilioni. Lengo kuu ni kuimarisha mnyororo wa thamani ya mafuta na gesi asilia kwa kutengeneza miundombinu inayotakikana. Programu hii itatekelezwa kupitia miradi mitatu na kwa mwaka 2023/2024, imepangiwa jumla ya TZS 11.0 bilioni kutoka Serikali.

***Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR)***

Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) umeanza mwaka 2022/2023 kwa lengo la kujenga kituo cha uhifadhi wa taarifa za mafuta na gesi asilia. Mradi huu wa miaka mitano (2022-2027) unatarajiwa kugharimu kiasi ya TZS 43.36 bilioni. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 4.0 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha ununuzi wa vifaa na vitendea kazi pamoja na kufanya marekebisho ya chumba kinachotumika kwa ajili ya kituo cha muda cha uhifadhi wa Taarifa;
ii. Kuendesha mafunzo ya usimamizi wa Taarifa kwa wataalamu wa Usimamizi wa Taarifa wa Mamlaka;

iii. Kuajiri Mshauri Elekezi kwa ajili ya kutoa huduma za kitaalamu za ujenzi zikiwemo usanifu na uchoraji ramani;
iv. Kulipia fidia mali na vipando vilivyopo katika eneo la ujenzi wa mradi; na
v. Kuanza ujenzi wa kituo cha uhifadhi taarifa.

***Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Gesi Asilia na Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi (LPG)***

Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Gesi Asilia na Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi (LPG) umeanza mwaka 2022/2023 na unatarajiwa kukamilika 2026/2027 kwa gharama ya TZS 70.0 bilioni. Lengo la mradi huu ni kujenga bohari ya gesi yenye ujazo wa 1,500MT katika eneo la Mangapwani Zanzibar. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Usafishaji na uwekaji sawa wa eneo la ujenzi wa bohari;
ii. Malipo ya awali kwa Mshauri Elekezi wa mradi; na
iii. Ujenzi wa bohari kwa awamu ya kwanza.

***Mradi wa Ujenzi wa Bohari ya Mafuta Mangapwani Zanzibar***

Mradi wa Ujenzi wa Bohari ya Mafuta Mangapwani Zanzibar una lengo la kuwepo kwa bohari ya uingizaji wa mafuta na ufanyaji wa biashara ya mafuta Zanzibar. Mradi huu ni wa miaka mitano (2022/23 – 2026/27) unatarajiwa kugharimu kiasi ya TZS 60.0 bilioni ambapo kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 3.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Usafishaji na uwekaji sawa wa eneo la ujenzi wa bohari;
ii. Malipo ya awali kwa Mshauri Elekezi wa usimamizi wa ujenzi; na
iii. Ujenzi wa bohari kwa awamu ya kwanza.

***Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu***

Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha shughuli za uchumi wa buluu kwa kuendeleza uvuvi mdogo mdogo na wa bahari kuu na ufugaji wa mazao ya baharini kwa maendeleo endelevu ya

uchumi wa buluu. Mradi huu wa miaka mitano (2022-2027) unatagharimu USD 30 milioni zinazotarajiwa kutolewa na Mshirika wa Maendeleo ambapo kwa mwaka 2023/2024, jumla ya TZS 3.5 bilioni zimepangwa kutumika.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujenga uwezo kwa wadau wa sekta ya Uchumi wa Buluu; na
ii. Kushirikisha jamii katika usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

***Ujenzi wa Diko na Soko la Kisasa***

Mradi wa Ujenzi wa Diko na Soko la Kisasa una lengo la kuwawezesha wavuvi kuweza kupata huduma za msingi za bandari na masoko kwa kuwajengea diko na soko la kisasa katika eneo la Kama–Unguja. Mradi huu ni wa miaka miwili (2023/2024 – 2024/2025) utagharimu jumla ya TZS 15.0 bilioni na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 13.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa upembuzi yakinifu; na
ii. Kuanza ujenzi wa diko na soko la kisasa - Kama.

***Mradi wa Ujenzi wa Bandari za Uvuvi***

Mradi wa Ujenzi wa Bandari za Kisasa za Uvuvi umeanzishwa kwa lengo la kuwawezesha wavuvi kupata huduma za msingi na urahisi kwa uwepo wa masoko na bandari za uvuvi nchini. Mradi ni wa miaka miwili (2023/2024 – 2024/2025) unatarajiwa kuanza na ujenzi wa bandari katika eneo la Mangapwani ambao utagharimu kiasi ya TZS 25.0 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa TZS 10.5 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Mangapwani.

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za Baharini***

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za Baharini ni wa miaka miwili (2023/2024-2024/25) umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya maabara ya uthamini wa ubora wa bidhaa za baharini. Mradi huu unatarajiwa kutumika kiasi cha TZS 4.0 bilioni

hadi kukamilika kwake na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 4.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ukarabati wa vyumba vya maabara ya vimelea, kemia na mazingira;
ii. Ununuzi ya vifaa vya maabara ya uthamini wa bidhaa za baharini;
iii. Kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wataalamu wa maabara juu ya matumizi ya vifaa na utendaji kazi bora wa maabara kwa kufuata viwango vya kimataifa;
iv. Kutengeneza Mfumo wa TEHAMA wa Uthamini wa bidhaa za baharini;
v. Kutengeneza miongozo ya kutambua ubora na uthamini wa bidhaa za baharini; na
vi. Kutengeneza mtambo wa kuharibu taka (Incineration plant).

***Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini***

Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini umeanza mwaka 2023/2024 kwa lengo la kuwawezesha wakulima na wasindikaji wa mazao ya baharini kufikia maendeleo endelevu ya mnyororo wa thamani. Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2022-2027) kwa gharama ya USD 5.5 milioni kutoka kwa washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa kiasi cha TZS 3.4 bilioni kwa ajili ya utekelezaji.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha mashamba nane ya majaribio ya mwani/majongoo bahari;
ii. Kuanzisha vitalu vinne vya mwani na majongoo bahari;
iii. Kutoa mafunzo kwa wanawake 8,000 wakulima wa majongoo bahari;
iv. Utoaji wa vifaa kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini; na
v. Usimamizi na uratibu wa shughuli za mradi.

***Mradi wa Maendeleo Endelevu ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini***

Mradi wa Maendeleo Endelevu ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeanzishwa kwa lengo la kuendeleza uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini kwa kwa maendeleo ya uchumi wa buluu nchini. Mradi utatekelezwa kwa

kipindi cha miaka sita (2023/2024-2028/2029) utagharimu kiasi cha TZS USD 39 milioni na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa kutumia TZS 6.5 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari;
ii. Kuimarisha mfumo wa taarifa za pwani na bahari pamoja na ununuzi wa vifaa vya mawasiliano;
iii. Ujenzi wa majengo ya uhifadhi na utafiti; na
iv. Kuandaa na kupitia sera, sheria na kanuni.

***Mradi Jumuishi wa Kuhifadhi Ikolojia na Kuendeleza Uchumi wa Bahari Tanzania***

Mradi Jumuishi wa Kuhifadhi Ikolojia na Kuendeleza Uchumi wa Bahari Tanzania unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka sita (2023/2024-2028/29) kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu unaolenga usimamizi endelevu wa mazingira na rasilimali za mwambao kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo ambapo kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 3.5 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutangaza zabuni kwa ajili ya kutafuta mkandarasi wa kusimamia mradi;
ii. Kuwajengea uwezo watendaji kwa ajili ya usimamizi wa mradi;
iii. Kufanya mikutano ya kuthibitisha ripoti ya utekelezaji wa mradi;
iv. Kujenga uelewa kwa jamii kuhusiana na usimamizi endelevu wa mazingira kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi; na
v. Kutayarisha Mkakati na Mpango Mkuu wa ufugaji wa viumbe maji hapa Zanzibar.

***Mradi wa Bahari Maisha***

Mradi wa Bahari Maisha umeanzishwa kwa lengo la kujenga uwezo wa kitaasisi katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi Maeneo ya Bahari. Mradi huu ni wa miaka saba (2023/2024-2029/30) unatarajiwa kutumia USD 30 milioni ambapo kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 6.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuwajengea uwezo watendaji kwa ajili ya utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari;
ii. Kufanya tathmini ya kimazingira kwa maeneo ya bahari ili kuwa na taarifa za awali (baseline data);
iii. Kukusanya takwimu za hali ya mikoko, matumbawe na majani bahari katika eneo la Zanzibar; na
iv. Kuimarisha mfumo wa GIS kwa ajili ya matumizi ya mradi.

***Mradi wa Mashirikiano wa Usimamizi wa Bahari na Uvuvi kwa Nchi za Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFC)***

Mradi wa Mashirikiano wa Usimamizi wa Bahari na Uvuvi kwa Nchi za Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFC) ni mradi wa miaka mitatu (2023/2024-2025/26) utakaogharimu kiasi ya USD 149,716 kwa lengo la kuimarisha mashirikiano ya usimamizi wa bahari na kuboresha shughuli mbadala za jamii zinazoishi mwambao wa Bahari kwa Nchi za Kusini mwa Bahari ya Hindi. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa TZS 345 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kutoa mafunzo kwa vikundi 20 vinavyojishughulisha na ufugaji wa majongoo bahari kwa jamii iliomo katika eneo la hifadhi la PECCA;
ii. Kutoa vifaa vya kwa ajili ya ujenzi wa vizimba vya kaa kwa vikundi 20 katika eneo la hifadhi la PECCA;
iii. Kufanya ufuatiliaji wa shughuli mbadala zilizoanzishwa kwenye jamii ya PECCA na kuangalia juu ya upatikanaji wa masoko kwa bidhaa wanazozalisha;
iv. Kuhamasisha jamii ya PECCA juu ya ufugaji wa pweza;
v. Kutoa zana kwa ajili ya kusaidia ufugaji wa pweza katika shehia tatu zilizomo katika eneo la hifadhi PECCA;
vi. Kufanya ufuatiliaji katika shehia tatu zinazotekeleza ufugaji wa pweza; na
vii. Utafiti wa kuangalia maeneo muhimu ya ufugaji wa majongoo bahari na kaa tope pamoja na kuangalia maeneo ya ufugaji wa pweza.

***Mradi wa Utafiti wa Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii***

Mradi wa Utafiti wa Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii una lengo la kujenga uelewa kupitia kutoa ufadhili wa elimu ya juu kwa mashirikiano ya tafiti juu ya kudumisha uchumi, usalama wa chakula na maisha endelevu. Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2023/2024-2025/2026) kwa gharama ya USD 86,000 na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 198 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutoa udhamini wa kufanya tafiti katika sekta ya kuimarisha uvuvi hasa kwa wavuvi wadogo wadogo;
ii. Kusaidia shughuli za usimamizi na uendeshaji wa Taasisi; na
iii. Kutoa nafasi ya ufadhili wa masomo wa elimu ya juu.

***Mradi wa Kuongeza Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Usimamizi Jumuishi wa Rasilimali za Bahari na Uchumi wa Buluu Endelevu (ZAN BLUE)***

Mradi wa Kuongeza Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Usimamizi Jumuishi wa Rasilimali za Bahari na Uchumi wa Buluu Endelevu (ZAN BLUE) unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka sita (2023/2024-2028/2029) kwa lengo la kujenga uwezo katika kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa rasilimali za baharini. Mradi huu unatarajiwa kutumia kiasi cha USD 250,000 na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 230 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya tathmini ya ujuzi unaohitajika katika kufuatilia na kuchambua hali za mazingira ya baharini na mwambao;
ii. Kutayarisha miongozo ya kuyatambua maeneo muhimu ya mazalia ya baharini na kutekeleza mpango wa uhifadhi wa mazingira ya baharini;
iii. Kuongeza uwezo kwa Idara za SMZ na Taasisi zake juu ya kufuatilia na kuchambua hali ya mazingira ya baharini na mwambao;
iv. Kuongeza uwezo wa Idara za SMZ na Taasisi zake katika kuyatambua maeneo muhimu ya mazalia ya baharini na kutekeleza mpango wa uhifadhi wa mazingira ya baharini; na
v. Kuendesha mafunzo ya kuyatambua maeneo muhimu ya mazalia ya baharini na kutekeleza mpango wa uhifadhi wa mazingira ya baharini.

*Mradi wa Kuweka Mitambo ya Kuhifadhia Baridi*

Mradi wa Kuweka Mitambo ya Kuhifadhia Baridi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya kuhifadhia baridi kwa ajili ya kuwezesha uhifadhi wa samaki na kuwasaidia wavuvi katika kuendesha biashara kwa ufanisi. Mradi huu unatarajiwa kutumika USD 232,559 hadi kukamilika kwake na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa TZS 536 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa*

- Ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia baridi.

*Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Ukusanyaji wa Tozo katika Maeneo ya Hifadhi*

Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Ukusanyaji wa Tozo katika Maeneo ya Hifadhi unaofadhiliwa na Shirika la UNDP (Biofin Project) unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa tozo katika maeneo ya Hifadhi. Mradi huu kwa mwaka 2023/2024 unatarajiwa kutumia TZS 115 milioni kutoka Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kufanya tathmini ya utayari wa kulipa kwa watalii wanaoingia katika maeneo ya hifadhi;
ii. Kufanya tathmini ya malipo ya sasa ukilinganisha na maeneo mengine ya ukanda wa bahari ya hindi na kwengineko;
iii. Kuandaa marejeo ya viwango vya malipo katika maeneo ya hifadhi; na
iv. Kuwajengea uwezo wadau wa utalii kuhusu ukusanyaji wa tozo tarajiwa.

## 8.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Wizara hii inahusisha sekta kuu tatu (Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji) zenye jukumu la kusimamia ubora wa miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine. Kuendelea kwa sekta za ujenzi, mawasiliano na usafirishaji huongeza haiba ya miji na kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara imepangiwa jumla ya TZS 559.45 bilioni (TZS 235.45 bilioni kutoka Serikalini na TZS 324.00 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo) kwa utekelezaji wa programu nne na miradi miwili ya maendeleo.

***Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu***

Programu ya ujenzi wa barabara kuu imeanza mwaka 2022/23 na inahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 407.6. Kwa mwaka 2023/2024 programu itahusisha ujenzi wa barabara kuu mbalimbali ikiwemo barabara mpya na zinazoendelea na inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Programu hii ina lengo la kujenga kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani kwa barabara kuu za Unguja na Pemba. Programu itasaidia kwa kiasi kikubwa kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar sambamba na kuhuisha uchumi na uwekezaji kwa vile barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo ya usafirishaji ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na maeneo mengine ya kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 249.38 bilioni (TZS 75.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 174.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali***

i. Kufanya tathmini na ulipaji wa fidia kwa vipando na nyumba katika maeneo yatayoathirika na ujenzi;
ii. Kupeleka na kuondoa miundombinu wezeshi katika maeneo yanaotarajiwa kujengwa barabara;
iii. Usafishaji wa maeneo pamoja na kuanza uwekaji wa fusi na lami kwa baadhi ya barabara;
iv. Ujenzi wa mitaro pamoja na kuanza uwekaji wa lami kwa baadhi ya barabara; na
v. Uwekaji wa alama na taa za barabarani.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na na Washirika wa Maendeleo***

i. Kuanza ujenzi wa barabara ya Tunguu-Makunduchi km 53;
ii. Kuanza ujenzi kwa barabara ya Chake Chake-Mkoani km 43.5;
iii. Kuanza ujenzi wa barabara ya Fumba - Kisauni kilomita 12 pamoja na Airport spur; na
iv. Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake km 22.1;

***Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani***

Programu hii imeanza mwaka 2022/2023 na itahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Programu itasaidia kuunganisha mitaa na maneneo

mbalimbali na barabara kuu. Aidha, kukamilika kwa programu hii kutasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha mitaa na maeneo mbalimbali. Vile vile programu itasaidia kurahisisha usafirishaji wa mzigo na kuchochea ukuaji wa uchumi na kumairika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 44.0 billioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya tathmini pamoja na ulipaji wa fidia za nyumba na vipando vitakavoathirika na ujenzi;
ii. Usafishaji wa maeneo pamoja na kuanza uwekaji wa fusi na lami kwa baadhi ya barabara;
iii. Ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa lami kwa baadhi ya barabara zilizokwishaanza kujengwa; na
iv. Uwekaji wa alama na taa za barabarani kwa baadhi ya barabara za ndani.

***Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini***

Programu hii imeanza kutekelezwa mwaka 2022/2023 na imehusisha ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini. Kwa mwaka 2023/2024 programu hii itahusisha uimarishaji wa barabara kadhaa katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na itahusisha ujenzi wa barabara, ujenzi wa njia za wapita kwa miguu, uwekaji wa taa pamoja na ujenzi wa mitaro ya maji katika barabara za mijini. Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha ya miji yetu na kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 80.1 kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara kuu za njia mbili (Two lanes dual) ikiwemo barabara ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume –Kiinua Miguu (5.2 km), Kiembesamaki-Amani-Mtoni (Mkapa road) km 8.8, Kariakoo – Magomeni-Mwanakwerekwe Sokoni km 2.9, Kinazini (BOT) - Mtoni km 3.5 Amani Round about-Mikunguni- Kwabizredi km 2.6;
ii. Kuanza ujenzi wa miundombinu kwa barabara kuu za njia moja (single carriage way) ikiwemo barabara ya Mazizini –ZRB- Mombasa km 0.6 na

kituo cha Polisi Ng'ambo – Mfereji wa Wima;

iii. Kufanya ukarabati wa barabara ndogo ikiwemo barabara ya Mazizini kituo cha Polisi-Chukwani Jeshini, Mazizini-Vitambulisho-Soko la Samaki, Mazizini VP2-Migombani, Miembeni round about –Michenzani Jumba namba 1 na 9, Miembeni round about–Bomani - K/chekundu hospitali, Saateni - Kwalimsha - JKU, Jangombe-Matarumbeta, Gulioni Gapco-Makadara-kwa Abass Hussein, Kijangwani Posta-Mwembeladu hospitali-Miti Ulaya, Mtendeni-Michenzani, Michenzani Jumba nambari 10-Gongoni-Kisiwandui-Msikiti Mabati, Skuli ya Kisiwandui-Mskiti Mabati- CRDB –Maisara-welles – Haile Salassie skuli, Benbella skuli-Kikwajuni/Maisara-Kikwajunu Mau-Michenzani, Kinazini-Lumumba skuli-Zanroad-Lumumba ZECO-Saateni, Mtoni depoti-ZECO Power Station-Mtoni Kidatu, Mwembe Makumbi-Basra-Karakana-Mtopepo skuli;

iv. Kuanza ujenzi kwa barabara ndogo zisizo na lami ikiwemo barabara ya Rahaleo ZBC-Bizred-Michenzani ring roads, Mpendae planned area, Chukwani mwisho-Buyu, Kilimani bar-Jangombe, Kwakira-kituo kipya Uwanja wa Ndege, Mbweni afya-Madina-Mbweni matrekta, ZSSF Mbweni Estate-Mbweni Ruins-Mbweni BOT quater-Kiembe Samaki, Baraza la Wawakilishi Chukwani-Makamo wa Kwanza wa Rais, River Tiba –Chukwani Tuta, Faraja Skuli-Mboriborini, Masumbani tawi la Kilimahewa-Shaurimoyo skuli, Saateni JKU-Rserved Storage-Saaten tank la maji/Shaurimoyo skuli, Makadara Mfereji wa Wima & Associate, Darajabovu Mboriborini, Magazeti Press-Mkele, Msikiti Shurba-Mshelishelini-Matarumbeta, Muungano Muembe Mkali, Muungano-Sogea, Mnara wa Mbao-Migombani Garden and Walkways in Garden; na

v. Kuzifanyia matengenezo Round about ya Mwanakwerekwe na Amani pamoja na ujenzi wa njia za juu (fly over).

***Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege***

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya kimataifa. Kwa mwaka 2023/2024 programu itahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba na hatua za awali za ujenzi. Programu itahusisha ujenzi wa maegesho, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Aidha programu hii inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa

mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 160.0 (TZS 10.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 150.0 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali***

i. Kukamilisha tathmini pamoja na kulipa fidia kwa maeneo yatakayoathirika na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba; na
ii. Kufanya upembuzi yakinifu pamoja na kuanza hatua za awali za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Nungwi.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa na Washirika wa Maendeleo***

- Kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa uwanja wa ndege Pemba.

***Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani***

Mradi huu ulianza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2022/2023. Mradi unalenga kujenga bandari kubwa na ya kisasa ambayo itahusisha gati tano ikiwemo gati ya mizigo eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta, bandari ya uvuvi, pamoja na chelezo cha kukarabati meli, kuamilika kwa bandari hii kutasaidia kuimarika kwa usafirishaji kwa vile bandari hii itasaidia kupunguza msongamano uliopo katika bandari ya Malindi unaosababishwa na ucheleweshaji wa utoaji wa huduma. Serikali inatarajia kushirikiana na sekta binafsi katika ujenzi wa bandari hii. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa bandari hii kutasaidia kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo ya sekta uvuvi, biashara na viwanda. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na wawekezaji kutoka katika sekta binafsi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 20.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Upelekaji wa miundombinu ya maji, umeme na barabara;
ii. Kufanya tathmini pamoja na ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliokuwa hayajakamilishwa malipo yake; na
iii. Usimamizi, kufanya ufuatiliaji na tathmini.

***Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Mawasiliano***

Mradi huu unatarajia kuanza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2023/2024 kwa lengo la kuimarisha mifumo ya mawasiliano ambayo itarahisisha utoaji wa huduma mbalimbali kutoka Serikalini. Aidha, mradi utaimarisha mifumo mbalimbali ya Serikali inayotumika katika ukusanyaji wa mapato na huduma

nyengine ambazo zitasaidia katika makusanyo ya mapato ya Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 5.9 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya tathmini ya mkonga wa mawasiliano; na
ii. Kufanya matengenezo na uwekaji wa mkonga wa mawasiliano.

### 8.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Wizara ina jukumu la kusimamia utalii na mambo ya kale kwa kuibua na kuongeza vivutio vipya sambamba na kuitangaza Zanzibar kiutalii. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara hii inatarajia kutekeleza programu moja ya maendeleo yenye jumla ya TZS 7.0 bilioni kutoka Serikalini itakayosaidia kuleta mageuzi katika sekta ya utalii na mambo ya kale.

***Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria***

Sekta ya Utalii ni sekta ya huduma inayokua kwa kasi hapa Zanzibar ambapo hutoa fursa nyingi za ajira na kuongeza pato la Taifa. Programu ilianza mwaka 2017/18 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.0 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha eneo la Ras – Mkumbuu Pemba;
ii. Kuimarisha maeneo ya kihistoria ya Maruhubi;
iii. Kuimarisha maeneo ya mahamamu ya Kijichi, Kizimbani, Hamamni na Forodhani; na
iv. Kuimarisha maeneo ya kihistoria ya Mangapwani;

## 9. MIRADI YA MAENDELEO INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KUPITIA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Kulingana na mwelekeo wa mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatarajia kutumia TZS 7.2 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Shughuli za maendeleo zitakazotekelezwa kwa mwaka 2023/2024 kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ni pamoja na:-

i. Kukamilisha ujenzi wa masoko makubwa ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.
ii. Kuendelea na ujenzi na ukarabati masoko katika Wilaya mbali mbali za Unguja na Pemba;

iii. Kuendelea na ujenzi wa stendi, vituo vya kusubiria abiria, maegesho na njia za wapitao kwa miguu katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba; na
iv. Kuanza ujenzi wa ukumbi wa mikutano, vyoo vya skuli, bango la matangazo la kielektroniki, viwanja vya kufurahishia watoto vya Wilaya pamoja na ununuzi wa magari ya taka kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

## 10.UFUATILIAJI NA TATHMINI

Kwa mwaka 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar imepanga kusimamia kwa karibu masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo kupitia maeneo yafuatayo:-

i. Kuandaa Mkakati wa Mawasilianao wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026;
ii. Kushirikiana na sekta katika kuutumia Mfumo wa kielekroniki wa Ufuatiliaji na Tathmini (Electronic M&E System) kwa programu na miradi ya maendeleo ili kuleta matokeo kwa malengo makuu (goals), matokeo ya muda wa kati (outcome), muda mfupi (output), shabaha (targets) na viashiria vitakavyotumika kupima matokeo hayo;
iii. Kufanya ufuatiliaji kwa programu na miradi yote ya maendeleo itakayoingiziwa fedha;
iv. Kufanya tathmini kwa programu na miradi ya maendeleo inayoendelea (Output), itakayokamilika (Outcome) na iliyokamilika (Impact); na
v. Kuandaa Mapitio ya Mpango wa Maendeleo wa muda wa kati (ZADEP 2021-2023).

## 11. WASHIRIKA WA MAENDELEO

Washirika wa Maendeleo watakaochangia bajeti ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2023/2024 ni pamoja na mashirika ya kifedha kama vile: Adaptation Fund (AF), ADB, AfDB, BADEA, Benki ya Dunia, CITI BANK, DEUTCH BANK, EXIM BANK (INDIA), Global Fund (GF), Khalifa Fund na Kuwait Fund, SAUDI FUND (SF); Nchi Wahisani wa maendeleo ambao ni: AUSTRIA, CANADA, KOREA, NORWAY, OMAN, SWEEDEN na UAE; na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo: AMREF, EDF –EU, ENABEL, GAVI, GEF, Germany, Good Neighbour, GPE, IAEA, IFAD, IRISH EMBASSY, JICA, KFW, KOICA, USDA-USAID, NORAD, SIDA -DLI, STBF, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, UKEF, UN-WOMEN na FAO.

## 12. HITIMISHO

Kitabu hiki kinatoa Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024, vile vile kimeanisha maeneo ya kimkakati kwa kipindi mwaka 2023/2024.

Hivyo Wakuu wa Wizara, Taasisi na Idara za Serikali watakitumia kitabu hiki kama muongozo wa utekelezaji wa Programu na Miradi iliyoainishwa, kusimamia na kuratibu program na miradi hiyo. Aidha, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinatakiwa kuendelea na utaratibu wa kutayarisha na kuwasilisha Tume ya Mipango mtiririko wa fedha (Cash Flow) za programu na miradi kabla ya tarehe 10 mwezi wa Julai 2023 sambamba na kuwasilisha maombi ya fedha za utekelezaji wa shughuli za Programu/Mradi kila wiki ya mwanzo ya mwezi husika. Inasisitizwa kuwa uwasilishaji wa maombi ya fedha uambatanishwe na vielelezo stahiki kwa mujibu wa shughuli za programu au mradi kama ilivyokubalika Serikalini ikiwemo mikataba.

Ili kurahisha utekelezaji wa Mpango huu ulioanishwa katika kitabu hichi kwa ufanisi Mashirikiano makubwa yanahitajika kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika utoaji wa Taarifa za utekelezaji wa kazi zilizoainishwa. Taarifa za utekelezaji ziwasilishwe Tume ya Mipango ndani wiki ya pili ya kila robo mwaka (2023/2024). Taarifa hizo zitajumuisha utekelezaji halisi na matumizi ya fedha ambazo zitatakiwa kuwasilishwa kwa usahihi zikiwemo fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Aidha Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia zinashauriwa kuoanisha Mipango yao na mpango huu ili kuungana na juhudi za Serikali kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kurasa zifuatazo zina kiambatisho ambacho kinaonesha mgawanyo wa fedha za Programu na Miradi ya Maendeleo Kiwizara kwa mwaka 2023/2024 kwa fedha za Serikali na za Washirika wa Maendeleo.

**Kiambatisho Nam 1: PROGRAMU/MIRADI INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2023/2024 ("000")**

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **A01** | **OFISI YA RAIS - IKULU** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali | 2,400,000 | 2,400,000 | | | | 2,400,000 |
| | ii) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mhe. Rais | 1,600,000 | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **4,000,000** | **3,400,000** | | - | - | **3,400,000** |
| **A09** | **TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Nyaraka | | 4,500,000 | | | | 4,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | | **4,500,000** | | | | **4,500,000** |
| **A07** | **OFISI YA RAIS - KAZI NA UWEZESHAJI** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuimarisha Uwezeshaji Wananchi Zanzibar** | 27,600,000 | | | | | - |
| | **Mradi** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa | | 4,500,000 | KHALIFA FUND | 2,510,000 | | 7,010,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **27,600,000** | **4,500,000** | | **2,510,000** | - | **7,010,000** |
| **A08** | **OFISI YA RAIS - UCHUMI NA UWEKEZAJI** | | | | | | |
| | **Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji** | 15,100,000 | 3,500,000 | | | | 3,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **15,100,000** | **3,500,000** | - | - | - | **3,500,000** |
| **F01** | **OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | 92,200,000 | | | | | |
| | i) Ukamilishaji wa Ofisi za Serikali | | 19,044,000 | | | | 19,044,000 |
| | ii) Ujenzi wa Mji wa Serikali | | 55,078,000 | | | | 55,078,000 |
| | **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | | | BENKI YA DUNIA | | 22,810,000 | 22,810,000 |
| | **Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP)** | | 128,400 | NORWAY | 3,768,880 | | 3,897,280 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **Mradi** | | | | | | |
| | i) Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili | | 34,700 | AfDB | 1,691,273 | | 1,725,973 |
| | ii) Kuongeza Uwezo wa Kiutendaji | | | UNDP | 350,000 | | 350,000 |
| | iii) Ulipaji wa Madeni kwa miradi ya Maendeleo | | 144,000,000 | | | | 144,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **92,200,000** | **218,285,100** | | **5,810,153** | **22,810,000** | **246,905,253** |
| **F03** | **TUME YA MIPANGO** | | | | | | |
| | **Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar** | 4,000,000 | 2,000,000 | | 500,000 | | 2,500,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Usimamizi, Kujenga Uwezo na Kuoanisha Mipango ya Kisekta, Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, SDGs na African Agenda) | 300,000 | | | | | - |
| | ii) Uratibu wa Shughuli za Kupambana na | 800,000 | | | | | - |
| | iii) Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi | 6,988,539 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | iv) Uimarishaji wa Ufanisi katika Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa | | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **12,088,539** | **5,500,000** | | **500,000** | **-** | **6,000,000** |
| **F04** | **OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | |
| | i) Mpango Mkuu wa Takwimu Tanzania (TSMP | 500,000 | | WB | | 4,427,400 | 4,427,400 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **500,000** | **-** | | **-** | **4,427,400** | **4,427,400** |
| **G01** | **OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** | | | | | | |
| | **Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (Phase II)** | 528,155 | 750,000 | | | | 750,000 |
| | **Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria** | 1,152,000 | 250,000 | UNDP/ IRISH | 969,632 | | 1,219,632 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Kusaidia Kukabiliana na Kesi za Ukatili kwa Utoaji wa Huduma ya Haki ya Masuala ya Kijinsia kwa Wanawake | | | UN-WOMEN | 373,600 | | 373,600 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,680,155** | **1,000,000** | | **1,343,232** | **-** | **2,343,232** |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **G02** | **MAHKAMA KUU** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi *(ECMIS)* | 1,000,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa | 5,550,000 | 25,000,000 | | | | 25,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **6,550,000** | **27,000,000** | | - | | **27,000,000** |
| **D01** | **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kiwanda cha Ushoni cha Idara Maalum za SMZ | | 5,000,000 | | | | 5,000,000 |
| | ii) Mradi wa Zanzibar Salama | 7,400,000 | 20,000,000 | | | | 20,000,000 |
| | v) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi wa Masheha | | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **18,920,000** | **28,000,000** | | - | - | **28,000,000** |
| **D12** | **WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** | | | | | | |
| | Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili | 1,100,000 | 950,000 | | | | 950,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,100,000** | **950,000** | | - | - | **950,000** |
| **D04** | **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM | 3,000,000 | 2,500,000 | | | | 2,500,000 |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Uzamiaji na Uokozi | 2,100,000 | | | | | - |
| | iii) Mradi wa Uwekaji wa Rada | 9,320,000 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **14,420,000** | **2,500,000** | | - | - | **2,500,000** |
| **D06** | **KIKOSI CHA VALANTIA** | | | | | | |
| | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Mahanga ya KVZ | 3,170,000 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **3,170,000** | **1,500,000** | | - | - | **1,500,000** |
| **D03** | **CHUO CHA MAFUNZO** | | | | | | |
| | Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga - Chuo Cha Mafunzo | 2,232,650 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,232,650** | **1,500,000** | | - | - | **1,500,000** |
| **D02** | **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi waNyumba na Mahanga ya Kambi za JKU | 3,250,000 | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa JKU | 2,214,765 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,464,765** | **3,000,000** | - | - | - | **3,000,000** |
| **D05** | **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari - KZU | 4,000,000 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | ii) Mradi wa Ununuzi wa Magari ya Zimamoto | 2,000,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **6,000,000** | **3,500,000** | | - | - | **3,500,000** |
| **B01** | **OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS** | | | | | | |
| | i) Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira | 4,500,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | ii) Mradi wa Kuirithisha Zanzibar Kijani | | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | iii) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Jamii ya Pwani | | | AF | 774,521 | | 774,521 |
| | iv) Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko wa Tabianchi kwa kutumia Mfumo Ikolojia Vijijini (EBARR) | | | UNEP | 234,417 | | 234,417 |
| | v) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Maji Machafu katika Eneo la Msingini- Kichungwani Chake Chake Pemba. | | | UNEP | 192,245 | | 192,245 |
| | vi) Mradi wa Kuimarisha Jamii kwa Kuzingatia Ikolojia na Shughuli za Kujipatia Kipato kwa Wavuvi Wadogo Wadogo na Usimamizi wa Eneo la Hifadhi la Mkondo wa Pemba (PECCA) | | | UNEP | 249,829 | | 249,829 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **4,500,000** | **3,500,000** | | **1,451,011** | - | **4,951,011** |
| | **MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA** | | | | | | |
| | Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya | 3,637,825 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **3,637,825** | **1,500,000** | | - | - | **1,500,000** |
| **C01** | **OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI** | | | | | | |
| | **Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III)** | 100,000 | 100,000 | BENKI YA DUNIA | 2,902,023 | 14,644,434 | 17,646,457 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **100,000** | **100,000** | | **2,902,023** | **14,644,434** | **17,646,457** |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **H01** | **WIZARA YA AFYA** | | | | | | |
| | **Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar** | 513,352 | 550,000 | GF | 977,728 | | 1,527,728 |
| | **Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto** | 1,517,588 | 1,000,000 | UNFPA/GAVI/ STBF | 4,808,345 | | 5,808,345 |
| | **Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma** | 94,288 | 500,000 | AMREF/GF | 1,050,206 | | 1,550,206 |
| | **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya** | | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha huduma za Mama na Mtoto** | | | WB | | 1,789,671 | 1,789,671 |
| | **Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi** | | 20,000,000 | | | | 20,000,000 |
| | **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na** | | 20,000,000 | | | | 20,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Kuanzisha Bima ya Afya Zanzibar | 1,549,893 | | | | | - |
| | ii) Uimarishaji wa Mifumo ya Afya | | 10,000,000 | | | | 10,000,000 |
| | iii) Ujenzi wa kituo cha Afya Kizimkazi | | | URT | 4,000,000 | | 4,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **25,194,795** | **53,050,000** | | **10,836,279** | **1,789,671** | **65,675,951** |
| **H02** | **HOSPITALI YA MNAZI MMOJA** | | | | | | |
| | Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | 5,553,000 | | BADEA/SAUDI FUNDS/ KUWAIT FUNDS | | 10,000,000 | 10,000,000 |
| | Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospital ya Mnazi Mmoja | | 1,125,200 | | | | 1,125,200 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,553,000** | **1,125,200** | | **-** | **10,000,000** | **11,125,200** |
| **N04** | **KAMISHENI YA ARDHI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi | 1,000,000 | 4,550,000 | | | | 4,550,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,000,000** | **4,550,000** | | **-** | **-** | **4,550,000** |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **R01** | **WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Viwanda** | | | | | | |
| | i) Kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks) | 2,500,000 | 26,012,000 | | | | 26,012,000 |
| | ii) Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa | 4,500,000 | | | | | - |
| | **Mradi** | | | | | | |
| | i) Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar | 4,000,000 | 2,405,000 | | | | 2,405,000 |
| | ii) Uimarishaji wa Miundombinu ya Kiwanda cha Kusindikia Mazao ya Kilimo Zanzibar | | | KOICA | 30,606 | | 30,606 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **11,000,000** | **28,417,000** | | **30,606** | **-** | **28,447,606** |
| **K01** | **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | |
| | **Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu** | | 59,038,146 | ADB/ AUSTRIA/ BADEA/DLI/ WB/ GPE/ KOICA/ SIDA/ UNICEF | 25,765,867 | 46,430,000 | 131,234,013 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi | 10,496,239 | | DLI/GPE/WB/ USAID/GOOD NEIGHBOURS | 4,624,400 | 1,500,000 | 6,124,400 |
| | ii) Uimarishaji wa Elimu ya Lazima | 21,978,260 | 15,172,590 | GPE (DLI)/ KOICA/ SIDA/ WB | 1,180,000 | 1,000,000 | 17,352,590 |
| | iii) Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya | 4,500,000 | 4,760,000 | | | | 4,760,000 |
| | iv) Uimarishaji wa Elimu ya Juu | | 20,000,000 | AUSTRIA/WB | | 1,600,000 | 21,600,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **36,974,499** | **98,970,736** | | **31,570,267** | **50,530,000** | **181,071,003** |
| **J03** | **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo** | 7,000,000 | 33,000,000 | GERMANY/GIZ | 1,278,054 | | 34,278,054 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **32,737,261** | **33,000,000** | | **1,278,054** | **-** | **34,278,054** |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **L01** | **WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO** | | | | | | |
| | **Programu ya Umwagiliaji** | 500,000 | 500,000 | KOREA | | 31,200,593 | 31,700,593 |
| | **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo** | | | | | | |
| | ii) Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo | 5,000,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | iii) Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki | | | ENABEL | 514,000 | | 514,000 |
| | iv) Mradi wa Kilimo Tija | | | USAID | 2,340,000 | | 2,340,000 |
| | **Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao** | | | | | | |
| | i) Kupambana na Sumukuvu Tanzania | | | AfDB | 485,558 | | 485,558 |
| | ii) Kudhibiti Upotevu wa Mazao | 2,194,847 | | IAEA | 421,576 | | 421,576 |
| | iii) Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda | | | EDF EU | 8,562,680 | | 8,562,680 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula | | 22,500,000 | | | | 22,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **8,694,847** | **25,000,000** | | **12,323,814** | **31,200,593** | **68,524,406** |
| **H04** | **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Hifadhi ya Wazee | 3,000,000 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | ii) Mradi wa Kutokomeza Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana | | | EU/ UN WOMEN | 636,321 | | 636,321 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **3,000,000** | **1,500,000** | | **636,321** | **-** | **2,136,321** |
| **N03** | **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | | | | |
| | **Program ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar** | | | | | | |
| | i) Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | 3,500,000 | 11,154,964 | INDIA (EXIM BANK) | | 18,503,702 | 29,658,666 |
| | ii) Uendelezaji wa Visima vya Ras el Khaimah | 18,154,964 | | | | | - |
| | iii) Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar | 1,090,700 | 2,850,000 | INDIA (EXIM BANK) | | 11,385,000 | 14,235,000 |
| | iv) Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar | | | KFW/ Germany | 2,600,000 | | 2,600,000 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | v) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (ZUWDFIP) | | | JICA | | 9,961,650 | 9,961,650 |
| | vi) Mradi wa Kufanya upembuzi Yakinifu wa Rasilimali Maji | | | SIDA | 10,484,460 | | 10,484,460 |
| | vii) Mradi wa Ununuzi wa Chlorine, Usimamizi na Uangalizi Bora wa Maji | | | UNICEF | 75,000 | | 75,000 |
| | viii) Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar | | 10,500,000 | | | | 10,500,000 |
| | ***Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar*** | | | | | | - |
| | i) Mradi wa Nishati Jumuishi Zanzibar | | | SWEEDEN | 67,628 | | 67,628 |
| | ii) Kuimarisha Miundombinu ya Umeme | 8,229,000 | 17,000,000 | | | | 17,000,000 |
| | iii) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) | 6,500,000 | 7,200,000 | BENKI YA DUNIA | | 8,878,345 | 16,078,345 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **37,474,664** | **48,704,964** | | **13,227,088** | **48,728,696** | **110,660,749** |
| **L02** | **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi** | | | IFAD | | 11,921,033 | 11,921,033 |
| | **Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia** | 11,000,000 | | | | | - |
| | i) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) | | 4,000,000 | | | | 4,000,000 |
| | ii) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Gesi Asilia na miundombinu ya Usambazaji wa Gesi (LPG) | | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | iiii) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Bidhaa za Petroli iliyosafishwa na Usambazaji | | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | ii) Uanzishwaji wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara Uthamini wa Ubora wa Mazao ya | | 4,000,000 | | | | 4,000,000 |
| | iii) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini | | | KOICA | 3,400,000 | | 3,400,000 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | iv) Ujenzi wa Bandari za Kisasa za Uvuvi | 30,000,000 | 10,500,000 | | | | 10,500,000 |
| | v) Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | | | EU | 3,500,000 | | 3,500,000 |
| | vi) Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki | | 13,000,000 | | | | 13,000,000 |
| | vii) Mradi wa Bahari Maisha | | | CANADA/ UNDP | 6,000,000 | | 6,000,000 |
| | viii) Mradi wa Mashirikiano wa Masuala ya Bandari na Uongozi wa Uvuvi kwa Nchi za Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi | | | FAO | 345,545 | | 345,545 |
| | ix) Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii | | | NORAD | 198,488 | | 198,488 |
| | x) Mradi wa Tafiti wa Zan Blue | | | FINLAND | 230,800 | | 230,800 |
| | xi) Uwekaji wa Mitambo ya Kuhifadhi Baridi | | | KOICA | 536,746 | | 536,746 |
| | xii) Kuboresha Mifumo ya Ukusanyaji wa Tozo katika Maeneo ya Hifadhi | | | UNDP | 115,400 | | 115,400 |
| | xiii) Maendeleo Endelevu ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini (TASFAMP) | | | WB | 2,500,000 | 4,000,000 | 6,500,000 |
| | xiv) Mradi Jumuisihi wa Kuhifadhi Ikolojia na Kuendeleza Uchumi wa Bahari Tanzania | | | AFD-FRANCE | | 3,500,000 | 3,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **52,000,000** | **35,500,000** | | **16,826,979** | **19,421,033** | **71,748,012** |
| **P01** | **WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu** | 37,947,000 | 75,387,000 | BADEA/SF/ UKEF/ DEUTCH BANK | | 174,000,000 | 249,387,000 |
| | **Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani** | 30,000,000 | 44,060,000 | | | | 44,060,000 |
| | **Programu ya Matengenezo ya Barabara za** | 135,600,000 | 80,100,000 | | | | 80,100,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 8,000,000 | 10,000,000 | UKEF/CITI | | 150,000,000 | 160,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani | 8,000,000 | 20,000,000 | | | | 20,000,000 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/2023 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2023/2024 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | ii) Uboreshaji wa Mifumo ya Mawasiliano (Connectivity) | | 5,900,000 | | | | 5,900,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **226,147,000** | **235,447,000** | | **-** | **324,000,000** | **559,447,000** |
| **J01** | **WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria** | 7,500,000 | 7,000,000 | | | | 7,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **7,500,000** | **7,000,000** | | **-** | **-** | **7,000,000** |
| | **JUMLA YA KUBWA** | **682,540,000** | **886,000,000** | | **101,245,826** | **527,551,828** | **1,514,797,654** |
| | **JUMLA YA FEDHA ZA WAHISANI** | | | | | **628,797,654** | |
| | **LGA** | | **7,200,000** | | | | **7,200,000** |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | | | | **1,521,997,654** |